ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chake Chake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kwanza - Tarehe 06 Disemba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA NAIBU SPIKA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Kwanza nichukue fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa Nane wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 6 Disemba, 2017.

Napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu miswada ya sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 27 Septemba, 2017 mpaka tarehe 12 Oktoba, 2017.

Katika Mkutano huo wa Saba wa Baraza la Tisa la Wawakilishi, Baraza hili lilipitisha Miswada Miwili (2) ya sheria ambayo ni:-

1) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 na Kuanzisha Upya Mahakama ya Kadhi na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo; na

2) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Taifa la Biashara na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.
Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016; naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo yote niliyoitaja sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa wajumbe nawashukuru wote ahsanteni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili waRais:
Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 13 Oktoba, 2017.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali na kuweka Masharti Bora ndani yake na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6

Historia ya Wanamapinduzi na Majemedari

Mhe. Ussi Yahya Haji - Aliuliza:

Wakulima na wakwezi wa visiwa vya Unguja na Pemba baada ya kuchoshwa na utawala wa kidhalimu wa Kisultani pamoja na Ubeberu wa Kiingereza walifanya Mapinduzi kuung'oa utawala huo tarehe 12/01/1964 na kuweka Serikali ya wananchi ambayo inaendelea na itaendelea kuwepo.

a) Je Serikali ina mpango gani wa kuweka maelezo juu ya historia ya Majemedari na Wanamapinduzi 14 walioongozwa na Mheshimiwa Hayati Abeid Aman Karume katika makumbusho maalum.

b) Je, Serikali wanazijua na wanazingatia vipi familia za Majemedari na Wanamapinduzi hao na iwapo zinahudumiwa ni huduma gani hizo wanazopatiwa.

Mhe. Naiwa Waziri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 6 lenye vipengele (a) na (b) kabla naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua na kuthamini sana jitihada zilizochukuliwa na Majemedari 14 wa Mapinduzi waliojitoa kwa hali na mali kupigania Uhuru wa Taifa letu. Namuomba Mwenyezi Muungu awalipe mema kwa wema wao walioufanya uliopelekea nchi yetu hadi sasa kuwa huru baada ya Mapinduzi ya tarehe 12/01/1964.

Mhe.Spika, baada ya maelezo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuthamini juhudi za Majemedari 14 wa Mapinduzi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatunza Historia

ya Viongozi hao katika Kituo cha Makumbusho kilichopo Kilimani, Wilaya ya Mjini-Unguja. Aidha.Wizara yangu inaandaa utaratibu wa Kisheria wa kuanzishwa Makumbusho maalum kwa ajili ya kutunza kumbu kumbu za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa ambapo wananchi watapata fursa ya kutembelea na kusoma historia ya Nchi yetu.

(b) Mhe. Spika, Serikali bado haijaanzisha utaratibu rasmi wa kuzihudumia familia za Majemedari hao wa Mapinduzi, hata hivyo Wizara yangu inaendelea kusimamia utaratibu uliowekwa na Serikali wa kila ifikapo tarehe 07 April kuwaombea dua Majemedari hao na kuadhimisha siku hiyo ya Mashujaa wetu wote waliokwishatangulia mbele ya haki.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, hakuna jambo kubwa katika nchi kuliko historia ya kujua tulikotoka tulipo na tunakokwenda, katika ulimwengu wote utashuhudia baadhi ya maeneo kuna masanamu mbali mbali ya viongozi wanzilishi na wengineo, kwa kwetu tunashukuru Mzee Karume yupo Afisi kuu na Uwanja wa Ndege Pemba na kwengineko lakini suala langu lipo hapa.

Je, kwa kuzingatia umuhimu wa Mapinduzi yetu ya mwaka 1964 na hapo tukafanikiwa kufikia hapa tulipo na katika suala nililoliuliza katika kipindi kilichopita Serikali ina mpango gani wa kuanzisha ujenzi maalum wa makumbusho kwa ajili ya viongozi wetu wakuu na mambo mengineyo.

Je. Wizara pamoja na kusema kwamba yapo kilimani ambapo picha mbali mbali zinaonekana hivi Wizara kwa makusudi na kwa

kuwa hili jambo ni muhimu kwa sisi na vizazi vyetu ina mpango gani wa kuharakisha kujenga ujenzi wa jengo hilo la makumbusho, ili sisi wenyewe na vizazi vyetu waelewe tulikotoka na hapa tulipo.

Mhe. Naiwa Waziri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kijitoupele suala lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimejaribu kusema katika jibu langu la msingi lakini pia kama ambavyo tutaweza kwenda katika Hansard zetu nimeshawahi kujibu suali la namna kama hii wakati huo liliulizwa na Mhe. Machano, tunachokifanya Serikali kwa hatua za awali kwanza kutaka kuanzisha sheria, tutakapoanzisha sheria sasa ndio tutapelekea kuweza kukusanya ile historia yote tukaweza kuiweka katika sehemu moja. Lakini kwa sasa kumbu kumbu hizi zimekuwa zikigawanyika katika maeneo tofauti, lakini tutakapokamilisha mchakato wetu wa sheria ambao kwa sasa sheria ile ipo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, tutaweza kulifanya jambo hili au kulihaulisha jambo hili kwa mujibu wa sheria hatutalifanya tena kimazoea, tutalifanya jambo kwa kuzingatia muongozo wa kisheria unasemaje. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 94

Gharama za Malezi ya Vijana JKU

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Suleiman Sarahan Said)-
Aliuliza:

Kwa kuwa kwenye utekelezaji wa Programu ya Kundi D.02 kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara iliwasajili jumla ya vijana 1550 kwa lengo la kuwapatia mafunzo mbali mbali ya uzalishaji mali na uzalendo. Na kwenye kundi hilo hilo kwa mwaka wa 2016/2017, Wizara imewasajili jumla ya vijana 2,206 kwa lengo la kuwapatia mafunzo ya uzalendo, kilimo, mifugo na kadhalika na kufanya idadi ya vijana waliosajiliwa kwa lengo la kupatia mafunzo kufikia 3756 kwa vipindi viwili.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali imetumia kwa ajili ya kutoa mafunzo mbali mbali kwa vijana hao na wangapi ambao wamemaliza mafunzo hayo.

(b) Je, kati ya vijana hao wote, ni vijana wangapi ambao wamepatiwa ajira za Serikali.

(c) Je, ni nini lengo la Wizara la kuwaendeleza wale vijana ambao tayari Serikali imeshatumia fedha kuwapatia mafunzo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 94 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, tangu mwaka 2013 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kupitia JKU kwa ajili ya kuendesha shughuli za mafunzo ya vijana katika kada mbali mbali zikiwemo ufundi, uzalendo na uzalishaji mali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Jibu (a) Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017 Serikali ilitumia jumla ya Shs. 2,564,661,600/= kwa kugharamia mafunzo ya vijana wanaojiunga na JKU ampapo imefanikisha kuwasajili jumla ya vijana 3,756 ambapo jumla ya vijana 2,782 sawa na asilimia 74% ya vijana waliosajiliwa wamehitimu mafunzo ya ufundi na uzalishaji kwa kipindi chote hicho. Kati ya hao 2,107 wamehitimu mafunzo ya uzalishaji mali na 680 wamehitimu mafunzo ya ufundi.

Mhe. Naibu Spika, jibu (b) kati ya vijana hao waliohitimu hakukuwa na kijana aliyepatiwa ajira kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vya Zanzibar na vile vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hii inatokana na ukweli kwamba tangu mwaka 2015 hakujatolewa kibali cha uajiri na Serikali kuu kwa Idara Maalum ya SMZ na kwa upande wa vikosi vya SMT kwa vijana wa Zanzibar. Fursa hiyo hupatikana kule JKT.

(c) Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali kwa vijana hawa ni kuwajengea uwezo wa kujiajiri kupitia mafunzo mbali mbali wanayopatiwa wakiwa makambini kama vile kilimo, ufugaji kuku na ng'ombe wa kisasa. Hata hivyo msimamo wa Serikali zote mbili SMT na SMZ pale inapotokea fursa Serikalini huwapa kipaumbele vijana walioko JKU na JKT. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza Swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara kwa kuhakikisha kuwa vijana wetu wanaelekezwa katika maadili mema na kufikia malengo kwamba wajiajiri hapo baadae baada ya kupata mafunzo mbali mbali, na katika majibu tumeshuhudia tu kwamba kuna

vijana wameelekea katika uzalishaji mali na wengine ufundi mbali mbali.

Je, kwa kuwa vijana wetu hawa wanategemea sana msaada na wanategemea wawezeshwe Serikali ina mpango gani kupitia Halmashauri zetu kwa kutenga angalau asilimia 5% kwa ajili ya kuwaendeleza vijana wetu, imefikiria vipi kwamba kuhakikisha wanapomaliza vijana wetu hawa watapata fungu la kuwaendeleza katika maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mheshimiwa Mwakilishi kwenye swali namba 94 kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, na mimi nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa kuliona hilo kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuwasaidia vijana wetu katika nchi yetu, ni jambo zuri lakini naomba nitoe ufafanuzi kwamba Mhe. Naibu Spika, jambo la kuwawezesha vijana katika nchi yetu kuna taasisi maalum au kuna Wizara maalum ambayo imetenga bajeti na miundombinu pia ya miongozo mbali mbali ambayo inaonesha namna gani vijana wanaweza kusaidiwa.

Hivyo basi naomba kwa swali hili nisitoe maelezo ya ziada zaidi ila tu kwa upande wetu sisi kama Halmashauri nadhani mambo kama haya tunakuwa tunayafikiria lakini hili jukumu sio la kwetu kwa kitaasisi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu hayo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba Wizara inachukua vijana wengi ni kweli na mimi naunga mkono hilo kupitia JKU ili kupata mafunzo ya kujiendeleza kiuchumi na kimaisha, lakini pia vile vile na kutumia pesa nyingi za Serikali ili kuwapatia mafunzo vijana wale, lakini wanapotoka makambini bado hubakia mitaani na kuendelea kuwa hawana kazi yoyote. Lakini kuna taasisi nyingi ambazo ni za *Private Sector*, je huoni kwamba ipo haja ya kuwaunganisha nao ili kuhakikisha vijana wale wasibakie mitaani na zile pesa za Serikali zikaonekana kwamba zimetumika vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mwakilishi mahiri Mhe. Makame Ali Muwakilishi wa Jimbo la Ziwani kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba iko haja ya kuona ni namna gani vijana hawa tunawaunganisha kwa taasisi mbali mbali ili kuweza kupata fursa ili wasibakie katika mitaa na baadae kuja kuingia katika mambo mengine. Lakini pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, naomba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako Tukufu waisaidie Serikali katika kuona kwamba ni namna gani tunakuwa tunasimama kidete, kama ambavyo tunaendelea siku zote katika kuona tunatafuta fursa na kuona vijana wetu wanapata fursa mbali mbali zilizomo nchini. Sio kwa taasisi za Serikali tu bali pia na taasisi nyengine binafsi pia na mifuko yetu kama tunaona kwamba upo uwezekano basi pia tuweze kusaidiana kuweza kutafuta hizo fursa mbali mbali ili vijana wetu hapa nchini waweze kuitumikia na kupata faida na waweze kuondokana na hali hiyo ngumu ambayo Mheshimiwa Mwakilishi ameweza kuionesha.

Lakini kwa upande wa taasisi yetu Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba jukumu hili kubwa liko kwenye Wizara ya Uwezeshaji wa Wananchi, Kiuchumi ambayo ina jukumu hilo naomba vile vile tusaidiane katika kuona kwamba ni namna gani kwa upande wetu na sisi tunaona ni kiasi gani waheshimiwa viongozi wetu wa taasisi wanaweza kufanya kazi kubwa zaidi katika kufanikisha jambo hilo. Mheshimiwa Ahsante sana.

Nam. 95

Ukarabati wa Barabara za Ndani, Ununuzi wa Boti na Vifaa vya Kufanyia Doria

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza**:**

Kwa kuwa kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilikuwa na mpango wa kuzitengeneza barabara za ndani, pamoja na kununua boti na vifaa mbali mbali ambavyo vingetumika kwa Doria ambayo pia ingesaidia kupambana na wahalifu wanaofanya magendo ya Karafuu.

(a) Je, Wizara imeweza kutekeleza lengo la kununua boti hiyo na gharama ya boti hiyo ni kiasi gani.

(b) Je, kati ya barabara ambazo zimetajwa kwenye mpango huo zote zimefanyiwa matengenezo kama ilivyoelezwa, kama sivyo ni sababu gani ya msingi iliyopelekea kutokamilika kwa barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: -

Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 95 lenye vipengele (a) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla Serikali imeweza kununua boti za doria na mashine zake ambazo ziligharimu shilingi 110,000,000 kwa boti zote hizo na mchanganuo wa gharama za kila boti upo pale Mwakilishi atakapouhitaji atapatiwa na kwa sasa boti hizo ziko kwenye kazi ya kufanya doria kwenye maeneo mbali mbali hapa nchini .

(b) Mhe. Naibu Spika, katika mpango wa matengenezo ya barabara za ndani kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ilipanga kufanya matengenezo ya barabara ya Magogoni Kwamabata - Kinuni yenye urefu wa kilomita 2 kwa kiwango cha lami na matengenezo hayo yamekamilika na hivi sasa tunaendelea na matengenezo ya barabara ya Kinuni - Kijitoupele.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza Mheshimiwa nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo inafanya na zinaonekana, lakini pili niseme kama si bahati na mvua kuwa inanyesha basi mambo yake yote ya barabara zingekuwa tayari.

Lakini suala langu lipo hapa Mheshimiwa kwa kuwa vijana wetu wa doria kwenye boti ambazo zimenunuliwa wanafanya kazi nzuri na tumethibitisha kwamba tumeshuhudia wanashirikiana na Tanzania Bara kukamata karafuu na mambo mengine, hata kuokoa wananchi wetu wanaopotea kwenye bahari kutoka Tanga na Pemba.

Je, Wizara ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha kwamba inaongeza doria hata tukizingatia kwamba karafuu zinaibiwa kwa wingi kupelekwa sehemu za nje, hili labda imejipanga vipi tu kuongeza nguvu na kuondoa kabisa tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupelo, Mheshimiwa mahiri Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba nizipokee pongezi ambazo amezitoa Mheshimiwa Mwakilishi kwa namna bora ambavyo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum inavyofanya kazi niseme kwa ueledi mpana zaidi, Mheshimiwa nazipokea kwa niaba ya Wizara kama ni motisha kwetu sisi kuona kwamba tunaendelea kuwajibika kama vile malengo ya Serikali ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa kazi nzuri ambazo zimefanywa na ni namna gani ambavyo tunaweza tukaona kwamba tunaongeza juhudi katika kuhakikisha kwamba tunaongeza doria katika kudhibiti vitendo vya magendo ya karafuu na magendo mengine hapa nchini, Ofisi ya Rais kupitia Idara Maalum tunalo hili na jukumu letu la kawaida na ndivyo ambavyo tumekuwa tukifanya kila siku. Kwa hivyo juhudi hizi ambazo zimefanyika sasa hivi inaonekana kwamba tunaenda kutokana na hali ambavyo kwa kweliwafanya biashara au watu ambao ni wahalifu kila jinsi ambavyo wanatumia teknolojia nyengine na sisi tumekuwa tukijitahidi katika kuona kwamba tunaendelea kukabiliana nao kwa namna yoyote ile.

Kwa hivyo suala la kuongeza juhudi Mheshimiwa niseme kwamba ni jambo la kawaida na tutajitahidi ushauri wao kuuchukua kwamba pale tutakapoona kwamba pia kuna mazingira mengine tunaweza tukafanya kwa kadiri tuhakikishe kwamba ulinzi huo unaimarishwa, ili kuona kwamba karafuu zetu na bidhaa zetu hazitoroshwi kwa njia ya magendo.

Mheshimiwa niseme kwamba tunauchukua ushauri na tunaendelea kwa sababu ni wajibu wetu na nakushukuru sana Mheshimiwa Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri naomba kuweka *hansard* sawa Mheshimiwa Ali Suleiman Ali *(Shihata)* ni Mwakilishi wa Kijitoupele sio Pangawe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nammshukuru Mwenyezi mungu kukutana siku ya leo, baada ya hapo naishukuru na kuipongeza sana timu ya Taifa ya Zanzibar kwa kuweza kushinda magoli 3 kwa 1 katika mashindano ya *Challenge* dhidi ya Ruanda hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nipatiwe majibu yangu ya suala langu namba12.

Nam. 12

Kuaminiana Kwa Taasisi Kwenye Ubora wa Bidhaa

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali imeamua kuunda chombo madhubuti cha kukagua na kuangalia ubora wa bidhaa mbali mbali yaani *(ZBS)* na kwa kule Tanzania Bara *(TBS)*, hata hivyo, kumekuwa na changamoto za taasisi hizi kuaminiana katika kazi za ukaguzi na

kupelekea usumbufu kwa wafanyabiashara wa upande wa Zanzibar wanapopeleka bidhaa zao kule Tanzania Bara.

(a) Je, Serikali inalitambua hilo.

(b) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua gani katika kulitatua tatizo hilo.

(c) Je, ZBS inaithamini na kuitambua bidhaa inayotoka Tanzania Bara ambayo inakaguliwa na *TBS*.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kabla ya kumjibu swali lake naomba nichukue nafasi kwa niaba ya Mwenzangu Waziri wa Habari anayeshughulikia mambo ya Michezo, kupokea pongezi zake za hatua ya kwanza kwa timu yetu ya *Zanzibar Heroes* kufikia angalau hatua ya kwanza, na tunaomba dua sisi wote humu ndani kwamba safari hii kombe litabakia Zanzibar tutalisherehekea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Serikali imeunda chombo madhubuti cha kukagua na kuangalia ubora kwa bidhaa mbali mbali yaani *ZBS* na kwa kule Tanzania Bara *TBS* lakini kumekuwa na changamoto za taasisi hizi kutokuaminiana katika kazi za ukaguzi na kupeleka usumbufu kwa wafanya biashara kwa upande wa Zanzibar wanaopeleka bidhaa zao kule Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a),(b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Viwango Zanzibar *(ZBS)* imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 1 ya mwaka 2011, jukumu kuu la kusimamishwa taasisi hii ni kuandaa viwango pamoja na kusimamia matumizi ya viwango hivyo.

ZBS imeanza kazi zake za uthibiti ubora wa bidhaa kwa kuwapatia alama ya ubora ya *ZBS* kwa wazalishaji mbalimbali nchini na nje ya nchi ambao bidhaa zao zimekidhi matakwa husika ya viwango vya Zanzibar.

Aidha, *ZBS* imeanza utekelezaji wa ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi kwa kupitia mifumo mikuu miwili ya ukaguzi wa bidhaa hizo ambayo ni:-

- "*Pre export verification of conformity to Standards (PVoC)"* ambapo bidhaa hukaguliwa nje ya nchi kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini.
- "*Destination Inspection (DI)"* ambapo bidhaa hukaguliwa baada ya bidhaa kufika nchini na kabla ya kuingia.

Mhe. Naibu Spika, *ZBS* na *TBS* zimesaini makubaliano ya pamoja ya ushirikiano baina ya taasisi hizi ili kurahisisha biashara nchini.

Aidha, taasisi hizi mbili zimeunda kamati maalum ya wataalamu ambayo hukaa kila baada ya muda kujadiliana changamoto na kuzitafutia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua kuwepo kwa changamoto hii, na hili linatokana zaidi na bidhaa ambazo zinaingizwa nchini na baadae kusafirishwa

Tanzania Bara, kiuhalisia bidhaa zinazoingizwa nchini na baadae kupelekwa Tanzania Bara huwa zinafanyiwa ukaguzi na wakaguzi wa *ZBS (Physical Inspection),* na kwa vile taratibu za udhibiti ubora zikamilike ni lazima bidhaa ikaguliwe na ipimwe maabara kama inakidhi matakwa ya viwango husika. Hivyo basi ndio maana *TBS* huchukua sampuli na kwenda kuzipima bidhaa hizo maabara.

(b) Mhe. Naibu Spika, kupitia kamati ya pamoja ya waatalamu baina ya *ZBS* na *TBS* wamekubaliana kuhakiki mifumo ya uthibiti ubora na ukaguzi kwa taasisi zote mbili ili kutengeneza mfumo ambao utasaidia kuondoa changamoto hizi.

(c) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Afrika Mashariki ya *"Standardization, Quality Assurance, Metrology and Testing (SQMT) Act"* inawataka kila nchi kutambua alama ya ubora wa bidhaa zilizothibitishwa na nchi wanachama wa jumuiya hiyo ila haiwazuii nchi husika kuchukua sampuli za bidhaa hizo na kuzipima maabara ili kujiridhisha kuwa inakidhi matakwa ya viwango husika. Hivyo basi Zanzibar tunaitambua alama ya ubora ya *TBS.*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mubashara ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda nina maswali mawili ya nyongeza.

a) Kwa kuwa bidhaa nyingi zinazoingizwa hapa Zanzibar hufanyiwa ukaguzi kama ulivyosema na zinapopelekwa Tanzania Bara inafika wakati zinachukuliwa tena kwenda kuangalia. Je, kufanyika hivyo huoni kwamba ni kutoiamini ZBS viwango vyake vya ukaguzi.

b) Kwa nini Zanzibar hawazuii bidhaa zinazotoka Tanzania Bara pale Bandarini ili waweze kuchukua na wao sampuli kwa

ajili ya kujiridhisha na ukaguzi uliofanywa Tanzania Bara vinalingana vile vile, na baadae kuweza kuruhusu kuingia sokoni.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Abdalla Maulid Diwani lenye vifungu (a) na (b)kama hivi ifuatavyo:

Kama nilivyosema katika suala la mwanzo la msingi nilivyojibu nilisema kwamba kwa mujibu wa sheria za *East Africa Standard Metrology Act* kila chombo kinaruhusiwa kama hakijaridhika kufanya ukaguzi kwa bidhaa ambazo zinaingia katika upande ule. Mara nyingi hutokezea kwa bidhaa za Zanzibar zinapokwenda Bara wakafanya ukaguzi. Hiyo haina maana kwamba hawakiamini chombo chetu cha *ZBS* lakini wakati mwengine wanaweza kufanya hivyo kwa sababu sheria inawapa.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, tumelizungumza katika vikao mbali mbali na hivi juzi tulikuwa na kikao tukasema kwamba vyombo vya viwango cha Zanzibar cha SMZ bado kichanga na bado kuna maeneo mengine hawajaweza kufikia hali hii ambayo inatarajiwa ya kimataifa, ndio maana mkaona katika bajeti tuliyopitisha mwaka jana na mwaka huu tumeagiza vifaa vingi ili kuweza kujenga chombo chetu hichi kiwe imara na kiwe na uwezo wa kufanya mambo mengi ambayo wanatakiwa kuyafanyia ukaguzi hapa Zanzibar.

Katika mazungumzo yetu tumesema kwamba wajibu wa Chombo cha Muungano kama cha TBS ni kuwafanya na wenzao waliokuwepo Zanzibar vile vile wawe na uwezo kama walivyokuwa na uwezo wao, kwa sababu kuna baadhi ya ukaguzi ZBS wanapeleka Bara vile vile kufanyiwa ukaguzi kwa sababu maabara hayo hawana. Kwa hivyo suala hili zima kama nilivyosema kwamba sheria inawaruhusu lakini hutokezea mara

chache wanapokuwa wanapoona kwamba labda wajiridhishe zaidi katika suala zima la ubora.

Suala la pili kwamba Zanzibar nayo tuchukue hatua vile vile kuanza kuzuia mizigo inayotoka Bara, mimi nafikiri tutakuwa tunafanya *tit for tat* hiyo kwa kweli hii haijengi Muungano wetu. Naomba nikumbushe tu kwamba ZBS na TBS wametilia mkataba wa mashirikiano. Niseme kwamba chombo ambacho kinafanya vizuri sana katika vyombo vya Muungao vinavyoshughulikia masuala ya ubora na masuala ya kukuza biashara, ZBS na TBS wanafanya kazi vizuri sana.

Niongeze tu kwamba katika Bodi ni chombo peke yake ukilinganisha chombo hichi ZBS na TBS na kile chengine cha vyakula, ZBS na TBS wametiliana mikataba wa mashirikiano. Lakini vile vile utaona kwamba katika bodi ya TBS vile vile kuna wajumbe wawili kutoka upande wa SMZ ambao wanawakilisha mle katika Bodi. Mmoja akiwemo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi yetu ya ZBS ambaye anawakilisha Zanzibar katika chombo cha TBS.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu mahusiano yapo mazuri sana na wanafanya kazi vizuri sana na baada kikao cha kwanza tulichofanya hivi juzi cha Muungano tukifanya kikao chengine tutakuwa na uwezo wa kuona kwamba vyombo hivi vinakuwa karibu zaidi na vinasaidiana utaalamu vifaa na vile vile mafunzo mbali mbali ambayo ZBS wanahitaji wapate ili wafikie viwango hivyo ambavyo vinatakiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kuchukua fursa hii kwa heshima kubwa kumuuliza Mhe. Waziri wa Biashara kuhusu swali hili la ZBS na TBS.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nchi yoyote duniani inaendeshwa na biashara ndiyo inayojenga uchumi wa nchi. Sasa hivi wafanyabiashara wetu wamekuwa wanalalamika sana dhidi ya matatizo ya bidhaa zao zinazoingizwa Zanzibar.

Mhe. Waziri mzoefu ameeleza vizuri sana na mimi nilikuwa namsikiliza kwa makini sana, naomba nimnukuu, amesema kwamba ”ZBS na TBS imetiliana mkataba ya mashirikiano” yaani wa kufanya kazi kwa pamoja. Sasa hoja yangu huo mkataba wa mashirikiano kama upo na umetiliana saini ni lini utaanza ku-*practise* ili hili tatizo liondoke ili mfanyabiashara wa Zanzibar aweze kuingiza biashara yake Bara bila ya matatizo anayoyapata sasa hivi kwa sababu kinachotokezea sasa hivi kinawafanya wafanyabiashara wanakuwa hawawezi kufanya tena biashara na pia wanaitia mdomoni Serikali ya Zanzibar, wanautia mdomoni Muungano, inaongeza kera za Muungano. Sasa kama kuna mkataba wa mashirikino lini utaanza kufanya kazi ili hili tatizo liondoke.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimejibu katika swali la nyongeza la Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba mkataba umeshatiwa saini na umeshaanza kufanya kazi. Ndio maana ukakuta kama nilivyosema kuna wajumbe wawili kutoka SMZ ambao wanawakilisha SMZ ndani ya bodi hii ya TBS.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kama nilivyosema wanashirikiana vizuri sana wanakutana mara kwa mara. Hivi juzi wamekutana, linapotokea tatizo lolote ambalo linasababisha kutokuwa na msimamo wa pamoja wanakaa hizi timu mbili na wanashirikiana na wanatoa ufumbuzi. Kwa hivyo kama nilivyosema bado haijafikia hali ile ambayo kwamba inakuwa ni rahisi moja kwa moja mizito kutoka Zanzibar kwenda kule Bara moja kwa moja. Lakini nimesema pia jambo hili tumelizungumza kwenye vikao

vya Muungano, tumemaliza hivi karibuni na tumepanga tena kukutana sisi na timu za Bara za biashara zote.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la ZBS na TBS sio tu kama ndizo zinazosababisha bidhaa zinazosababisha bidhaa zinazokwenda Bara kukwama kuna mambo mengine ya ziada ambayo yanayosababisha bidhaa hizi kukwama, kwa hivyo tunataka tutizame yote tusiangalie mambo ya viwango tu lakini tuangalie mambo yote ambayo yanasababisha bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Bara zikakwama. Tumekubaliana kukutana mwezi huu nafikiri katika wiki mbili hizi tutakutana na timu nzima ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji kule Bara na kuweza kuwekeana utaratibu uliokuwa mzuri sana.

Niongeze tu kwa taarifa kwamba Chombo chengine ambacho Bodi ya Vyakula na Madawa, taarifa nilizokuwa nazo kwamba wameshasaini mkataba wa mashirikiano. Kama nilivyosema sio chombo kimo ni vyombo viwili na vile vile TRA na kwengine ndiyo ambao wanaosababisha matatizo ya biashara kuenda vizuri sana kule Bara. Kwa hivyo nadhani kazi hiyo tuseme tu kwamba baada ya vikao hivyo mambo mengi yatatanzuliwa na tutaweza kuona ubora zaidi katika uwezo wa wafanyabiashara Zanzibar kuingia katika soko la Bara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 89

Malipo ya Mishahara ya Walinzi wa Maskuli kwa Wakati

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny.Ali Khamis Bakari) - Aliuliza:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inastahili pongezi kwa kuweka walinzi katika Skuli za Sekondari kama vile Chwaka, Tumbe, Pandani, Utaani, Konde na Wawi n.k ili kulinda skuli na kutoharibiwa kwa vifaa vilivyomo na kwa kuwa Wizara jambo

hili waliwapa Wanajeshi Wastaafu (UMAWA) ili kutoa huduma hii kwa uadilifu na ufanisi.

Je, ni kwanini pesa za mishahara ya walinzi huwa hawapati kwa wakati na wanacheleweshewa na lini jambo hili litarekebishwa ili kuendana na kazi yenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa Wizara imeingia mikataba na Kampuni za ulinzi binafsi hasa za askari wastaafu kwa ajili ya kutoa huduma za ulinzi katika baadhi ya skuli za msingi na sekondari. Kampuni hizo zinatoa huduma kwa Pemba katika Skuli za Sekondari mpya zikiwemo Chwaka Tumbe, Wete Sekondari, Utaani, Konde na Wawi.

Wizara inafanya malipo ya jumla kwa Kampuni na wala sio kwa mlinzi mmoja mmoja kwa mujibu wa makubaliano yetu. Suala la kuwalipa mshahara walinzi ni suala la Kampuni binfasi.

Kuhusu kuchelewa kuzilipa Kampuni za ulinzi inatokana na fedha za malipo yao haziingizwi sambamba na zinapoingizwa fedha za fungu la mshahara. Malipo ya mikataba ya ulinzi yanatokana na fedha za fungu la matumizi mengineyo ambayo Wizara huingiziwa baada ya fedha za fungu la mshahara. Hatahivyo, Wizara inafanya kila juhudi za kuzilipa Kampuni za ulinzi kwa kadri fedha za fungu la matumizi mengineyo zinapoingizwa. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii, naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe.

Waziri. Niwapongeze kwa hatua hiyo ya kuanza ulinzi katika shule zetu hizo. Lakini kuna walinzi sio wanajeshi wala polisi katika hao walinzi wametoka uraiani. Je, walinzi hao wameshapewa mafunzo ya ulinzi na maadili ya kazi zao wanapokuwa kazini. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa walinzi ambao wanapitia Kampuni, hizi Kampuni zina taratibu za kutoa mafunzo maalum ya kiulinzi. Lakini kwa walinzi ambao hapo zamani Wizara ilikuwa inaajiri hawa haikuwa lazima kupata mafunzo hayo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naipongeza sana kwa kupeleka masuala haya ya ulinzi kwenye *private sector* kama hawa Umawa na mambo mengine. Lakini ni kulinda ni kuhakikisha kwamba vile vifaa vilivyopelekwa maskulini haviibiwi kama lililotokea pale maeneo ya Mauwani Kiwani. Lakini mishahara hii inapochelewa mpaka ikafika miezi minne au mitano, walinzi wale kuwa hawajapata posho au mshahara hatuoni kwamba ni tatizo linalowapelekea kwamba wanakata tamaa hadi siku nyengine kuacha kwenda kulinda pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kwamba kuchelewa kumlipa mtu yeyote ni tatizo na wala serikali haifurahii suala hilo. Ndio maana tukasema kwamba tutafanya kila jitihada inayowezekana

ili kuweza kampuni hizi kuzilipa fedha zao kwa wakati ili na wao pia waweze liwalipa walinzi wao kwa wakati. Ahsante.

Nam. 9

Malipo ya Fidia kwa Vipando na Nyumba kwa Wananchi

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:

Serikali imejitahidi sana kuwasaidia wananchi wake kwa kuwaletea maendeleo mijini na vijijini, na pia kuwalipa fidia kwa wale ambao wamekatiwa vipando au nyumba. Lakini bado wananchi wa Tumbi na Zawaridu Shehia ya Chumbageni mpaka leo hawajalipwa fedha zao za fidia baada ya kukatiwa vipando vyao na kuwekewa transfoma na mabomba makubwa ya maji.

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fedha hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 9 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara yangu inatambua kwamba ina jukumu la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaoathirika kwa kuharibiwa mali zao kutokana na kazi za ufikishaji wa miundo mbinu ya maji, umeme, ujenzi wa matangi katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba,

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda nimjulishe Mhe. Mwakilishi kwamba serikali inaendelea na zoezi la kuwapatia wananchi fedha hizo awamu kwa awamu kwa kadiri ya uwezo wa fedha unavyoruhusu kutokana na uwezo wa bajeti ya wizara ya kila

mwaka kupitia Mamlaka ya Maji, ambapo kwa mwaka huu wa fedha jumla ya TZS milioni mia nane zimetengwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia si tu kwa Tumbi na Zawadini katika Shehia ya Chumbageni bali hata na maeneo mengine Unguja na Pemba. Ahsante sana.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri karibu tu katika eneo hili la Chumbageni wanaotarajiwa kulipwa fedha hizi ni watu sita, lakini kwa bahati mbaya kuna mmoja Bwana Khamis Mohammed Khamis ambaye kuwa ni mgonjwa hakuweza kufika katika eneo lile, je ni lini atalipwa pesa zake zile tukizingatia yupo kitandani lakini anaona, anaweza kuweka saini lakini pia ana kauli yake nzuri. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjimbu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Nimwambie tu kwamba tutalifuatilia na atalipwa haki yake. Ahsante.

Nam. 52

Uendelezaji wa Eneo la Makangale kwa Utalii

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa eneo la ukanda wa Makangale lilitengwa makusudi kwa ajili ya uwekezaji wa Mahoteli katika mwaka 1990, na kwa kuwa Serikali iliyapima maeneo hayo yote kwa ajili ya kuyatambua, na kwa sababu maeneo mengi ya Makangale yapo wazi hayaendelezwi kwa mujibu wa lengo lililokusudiwa.

(a) Je, Wizara imevipima viwanja vingapi kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli kutoka Serikalini kutangaza mpango huo.
(b) Je, ni hati au "*lease*" ngapi zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa hoteli huko Makangale.
(c) Je, ni hoteli ngapi za kitalii ambazo zimeshajengwa ambazo zinafanyakazi na ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali kwa watu waliopewa viwanja na wameshindwa kuviendeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 52 lenye vipengele (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la Makangale limepangwa na kutengwa kwa matumizi ya uwekezaji wa utalii. Hata hivyo ukanda huo pia una rasilimali ya msitu wa asili jambo ambalo linashurutisha aina ya uendelezaji wa sehemu hiyo kuwa *Eco-Tourism.*

(a) Mhe. Naibu Spika, Wizara imepima maeneo 39 kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli tokea serikali kutangaza Mpango wa Ukanda wa Utalii wa mwaka 1995.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali imekodisha na kutoa Mikataba ya Ukodishaji Ardhi 12 kwa ajili ya uwekezaji wa utalii na Mkataba 1 kwa uwekezaji wa mnara wa mawasiliano katika eneo hilo.

(c) Mhe. Naibu Spika, jumla ya hoteli 5 zimeshajengwa na zinafanya kazi katika eneo hilo. Aidha, serikali inachukua hatua za kuwabaini wawekezaji ambao hawakuendeleza maeneo waliyokodishwa na hatua ya kuwapa indhari na hatimae kuwafutia

zitachukuliwa kwa miradi ambayo haijatimiza masharti ya upewaji wao. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri napenda nimuulize kwa kuwa maeneo ni 39 yaliyopimwa na yaliyotolewa *lease* 12 na hoteli ni 5 pamoja na ya Mnara ukiyafanyia hesabu yatabakia maeneo 21 ambayo hayo hayana *lease* wala hayajaendelezwa.

a) Ikiwa maeneo yote hayo hayana *lease* wala hayajaendelezwa serikali haioni kwamba inapoteza mapato yake bure au itakuwa ni ipi ile faida ya kuyapima na kuyaweka kwa ajili ya uwekezaji.

b) Lakini pia ni jambo la kusikitisha kusema kwamba itafanya utaratibu wa kuyatambua. Ni lini sasa itayatambua hayo maeneo ambayo wawekezaji hawajayaendeleza ni lini. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kukaa maeneo bila ya uwekezaji hayaingizi kwa maana hiyo ni hasara, lakini wale ambao wamepewa na bado hawajafata masharti ya upewaji wao kama nilivyokuwa nimesema mwanzo watapewa indhari na hatimaye ifutwe kabisa. Lakini ni mambo ya kisheria ni lazima tufuate sheria, sasa sheria vile ambavyo itakuwa inatuelekeza basi ndivyo tutafuata. Kwa hivyo baada ya kukamilika ufuataji wa sheria utaona matokeo yake. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kunamayatima wamechukuliwa *plot* yao katika eneo la Makangale na mayatima wale wakafuata *procedure* zote wamechukuliwa na watu wazito wakafuata *procedure* zote za Serikali za malalamiko na Serikali kuwaambia wachague eneo moja na wakachagua. Lakini mpaka leo zaidi ya mwaka wa 10 hawajapata chochote mpaka sasa. Je, serikali ipo tayari kukaa na mimi pamoja na wale waliodhulumiwa mayatima kuweza kulitatua suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kwa kusema kwamba Wizara yangu ipo tayari kukaa nae na hao watoto yatima kwa kulitatua hili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa naomba sana kwenye *briefing* tulizungumza suala la wakati tulionao ni mgumu sana, ndio maana leo mnaniona nakatisha katisha najua watu wana hamu sana ya kuuliza maswali, lakini muda hatuna wa kutosha na maswali ni mengi mno, kwa hivyo mtu anataka kuuliza swali ajitayarishe na mapema ili niweze kumuona mapema nimpe nafasi ya kuuliza. Tunaendelea.

Nam. 97

Ufinyu wa Tanuri la Kuchomea Taka Katika Hospitali ya Chake Chake

Mhe. Zulfa Mmaka Omar (Kny Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza:

Serikali inastahili pongezi kwa jitihada zake za kuboresha huduma za afya katika Hospital ya Chake, ambako kuna tanuri ya kuchomea takataka za Hospitali *(Incinerator)* baada ya kufanyiwa matengenezo kutokana na agizo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wakati alipotembelea hospitali hiyo. Lakini bado taka zinatupwa ovyo na nyengine kuchomwa katika mashimo yaliyochimbwa katika maeneo ya wazi karibu na tanuri hilo na kusababisha kuzagaa kwa taka na kuleta harufu mbaya ya moshi wa sumu katika maeneo hayo.

(a) Je, kuna tatizo gani linalosababisha tanuri hilo kutotumika ipasavyo.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga tanuri kama hilo katika eneo muafaka kwani eneo lililopo tanuri hilo ni katikati ya mji wa makaazi ya watu.

(c) Je, Serikali haioni kuendelea na uchomaji huo na kutoa moshi wa sumu huenda ikaleta maradhi mengine yasiyo tarajiwa.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na wazima leo, kuja hapa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa mara nyengine tena.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake Mhe. Suleiman Sarahan Said ambalo limeulizwa na Mhe. Zulfa kwa niaba yake nambari 97 lenye vipengele (a), (b), (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika Serikali imepokea pongezi za Mhe. Sarahan katika kufanya huduma za afya kuwa bora zaidi hapa Zanzibar yaani Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, tanuri la kuchomea taka katika Hospitali za Chake chake kwa sasa linafanya kazi, ingawa baadhi ya wakati kunajitokeza changamoto za kiutendaji zinazohitaji matengenezo ya hapa na pale na ya mara kwa mara na pia gharama za uendeshaji wa tanuri hilo.

Hata hivyo, Wizara imepokea ushauri wa Mhe. Suleiman Sarahan na kuzingatia kuwa kuna haja ya kutafuta sehemu nyengine muwafaka ya kujenga tanuri jengine kubwa zaidi na la kisasa ambalo linaweza kufanya kazi hiyo ya kuchoma taka, pale Wizara itakapopata fedha basi ushauri huo utazingatiwa na kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara pia inatambuwa kuwa Hospitali ya Chake Chake sasa iko katikati ya mji na inazunguka makaazi ya watu, hivyo swali la moshi kuleta athari kwa jamii linadhibitiwa ipasavyo naomba nitamke moshi unaotoka pale si wenye sumu wala dhara yoyote kwa wananchi na uchomaji wa taka unaofanyika pale ni taka zile za *organic* na sio *chemical.* Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Zulfa Mmaka Omar swali la mwanzo la nyongeza.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla ya hiyo naomba nimwambie Mhe. Waziri kwamba swali hili si geni kwako na tukiangalia hata mimi si mara moja wala mbili nishawahi kukufata na kukuambia kwamba suala la taka taka

kutupwa ovyo katika Hospitali ya Chake Chake linatukera hasa vijana tunokwenda sehemu ile kwa ajili ya kufanya mazoezi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika swali langu Mhe. Waziri katika Hospitali ya Chake Chake niseme unafahamu kwamba ni *centre* ya watu wa Pemba, na ile ni hospitali inatumiwa na watu wengi sana kwa ajili ya kwenda kupata matibabu. Lakini la kusikitisha Mhe. Waziri hivi juzi juzi tu kaenda mgonjwa pale kufanyiwa *operation* ambaye alihitaji kupata chumba cha utulivu kwa ajili ya afya yake na alikosa sehemu ile na kwa bahati mbaya sana yule dada alipoteza maisha niseme kwamba kwa bahati mbaya kwa sababu alikosa utulivu katika hospitali ile. Pia tunaona kwamba viongozi maalum ambao wanakwenda katika hospitali ile Mhe. Waziri tukiona hata humu katika Baraza letu kuna viongozi ambao walilazwa katika Hospitali ya Chake Chake na hatimaye kulazwa katika chumba cha madaktari ambacho hakiko salama kwa kulazwa viongozi wale.

Jee, Mhe. Waziri huoni suala hili la kukosa sehemu maalum ya kulazwa viongozi maalum wa Serikali pia wagonjwa ambao wanahitaji utulivu kukosa sehemu ile huoni kwamba ni jambo la lazima, pia ni kukosa haki zetu viongozi ambao tunakwenda katika Hospitali ile.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Zulfa swali lake zuri sana alilouliza na kunisaidia kutoa baadhi ya ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza suala la taka naomba niseme kwamba lile tanuri lilioko pale ni dogo sasa hivi na limeshazidiwa kwa sababu hospitali ya Chake Chake imeanza kuwahudumia wananchi wengi zaidi, na kwa bahati mbaya sana tungependelea wananchi wangekuwa wanatumia Hospitali ya Abdalla Mzee lakini kutokana na umbali bado Hospitali ya Chake Chake

inaongoza kwa kupokea wagonjwa wengi zaidi kuliko hospitali nyengine yoyote Kisiwani Pemba, kwa hiyo Abdalla Mzee bado inapokea wagonjwa wachache na hii ni kutokana na umbali na masuala la usafiri.

Kwa hiyo pale hivi sasa kwa kweli Hospitali ya Chake imezidiwa na ina wagonjwa wengi na kila kukiwa na wagonjwa wengi ndipo taka zinapozidi na lile tanuri lishakuwa dogo. Kwa hivyo kuna kila haja ya kujenga tanuri kubwa zaidi kwa sababu muda wa uchomaji wa zile taka pia nao unakuwa mrefu ni taka nyingi sana na lazima taka za mwanzo ziunguwe ndio ziwekwe taka nyengine.

Kwa hivyo hilo naomba nimwambie Mhe. Zulfa kwamba Serikali imetenga Shilingi milioni 350,000,000/= katika bajeti hii iliyopitishwa kwa ajili ya utanuzi na ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Chake pia bahati nzuri tumefanya mazungumzo na wafadhili ambao wanatusaidia hivi sasa kuchora ramani ya baadhi ya maeneo ya Hospitali ya Chake Chake na kutafuta nafasi muafaka ambayo tutaweza pia kutanua huduma.

Kwa hiyo majengo mawili pale Hospitali ya Chake Chake yatabomolewa na kuwa ya ghorofa na jengo moja ni la *maternity* pamoja *female ward* na jengo la pili ni la *paediatric* la watoto bahati nzuri sasa hivi tuko katika mchakato wa kukamilisha ramani na hayo yote yakisha kamilika tunatoa tenda rasmi kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kujenge majengo hayo mawili kwa pale Hospitali ya Chake Chake.

Naomba pia nikubaliane na Mhe. Zulfa kwamba kuna ufinyu wa nafasi hivi sasa na ni kweli pale alipoumwa VIP alilazwa kwenye chumba cha daktari, ni kweli kabisa na hii inatokana na ufinyu wa nafasi naomba tuvumiliane kwa bajeti hii tulipata tutakwenda nayo ili tutakapopata hizo wodi mbili zile wodi za zamani zitaweza kutoa huduma na kufanyiwa ukarabati ambao utakuwa

bora zaidi kwa kutoa huduma kwa VIP wanapopata matatizo ama pia wagonjwa wa kawaida na nitoe tamko hilo Mhe. Naibu Spika.

Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa mimi nafasi ya kuuza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nimpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo nilimsikiliza kwa makini na alisema kwamba kuna upatikanaji wa milioni 300,000,000/= ambazo zitakarabati hospitali pamoja na mambo mengine, hasa mimi nilikuwa nimuulize tu swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Jee, pesa hizi tayari zishapatikana upatikanaji wake yaani ukarabati wake ni lini utaanza ili kuweza kuondoa usumbufu huu ambao wananchi wanaupata.

Mhe Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Pesa hizi tayari zimeshatengwa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Afya kwa ajili ya Hospitali ya Chake Chake Pemba.

Kwa hiyo naweza kusema zikishapatikana tatizo lililokuwepo lilikuwa hatujakamilisha masuala ya ramani na masuala ya kiufundi ambayo hivi sasa yanafanyanyiwa kazi na ndani ya muda mfupi yatakamilika.

Nam. 14

Kukosekana kwa Mwandishi wa Habari za Mawio Wilaya ya Mkoani

Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Aliuliza:

Kwa kuwa habari za mawio zinazotolewa asubuhi na ZBC Redio zinatoa matokeo ya habari mbali mbali zinazotokea ndani ya shehia za Unguja na Pemba, lakini habari hizi kwa upande wa Wilaya ya Mkoani hazisikiki.

a) Je, kuna sababu gani zinazosababisha kukosekana mwandishi wa habari za mawio Wilaya ya Mkoani.

b) Kukosekana kwa mwandishi wa habari za mawio katika Wilaya hii Wizara haioni inawanyima haki ya kupata habari muhimu zinazotokea ndani ya Wilaya hiyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 14 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ZBC haina waandishi maalumu walioajiriwa kwa kazi ya kuandikia habari za mawio, hivyo habari za mawio hutumwa na watu wa maeneo mbali mbali wanaoguswa na matukio matukio mazito na muhimu kwa jamii zetu yanayotokea katika maeneo yao au waandishi wa taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi mfano wa waandishi hao ni Masanja Mabula, Asha Hamad, Suleiman Rashid, na Kauthar Is-haq na wengi wengineo. Vile vile habari nyingi za mawio zinatolewa na waandishi wa kujitolea ambao hulipwa kwa kila habari wanayotoa na kwa vile upande wa Pemba hawako wengi waandishi wa aina hiyo sababu hizi zinapelekea kuonekana kunakosekana waandishi maalum kwa habari za mawiyo ndani ya Zanzibar na baadhi ya Wilaya ikiwemo Wilaya ya Mkoani.

b) Mhe. Naibu Spika, ZBC inakubaliana na hilo, analolizunguza Mhe. Mwakilishi kwamba ni muhimu Mkoani nako kuwa na waandishi wa habari za mawiyo na ZBC itaendelea kutafuta uwezekano wa kuwatafuta wawakilishi wa kuripoti habari hizo katika maeneo yanayokosa uwakilishi kwa sababu tatizo hilo sio la Mkoani peke yake, lakini pia tunaomba mashirikiano kutoka kwa wanajamii wote wa Pemba na Unguja wenye uzalendo wa dhati kwa jamii yetu wawe wanatoa taarifa za matukio hasa matukio mazito, matukio muhimu na matukio yenye kuelimisha yanayotokezea kwenye maeneo yao ambayo ni muhimu kwa jamii kuyasikia au kuyaona na kuyaripoti kwa njia ya simu au kwenda moja kwa moja kwenye vituo vyetu vya habari kwani kufanya hivyo kwa watu hao kutaongeza idadi ya matukio yanayoripotiwa kuweza kusikika na vile vile kuisaidia Serikali na vyombo vyake husika kuweza kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria za nchi zinavyoeleza.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi tena ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali dogo tu la nyongeza.

Ni sababu gani zinazosababisha Wizara kutowaajiri Waandishi wa Habari za Mawiyo wakati wanafanya kazi za kuelimisha jamii kwa matukio mbali mbali yanayotokea katika Shehia zetu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mheshimiwa sikusikia vizuri naomba arejee swali lake, sikusikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Tatu Mohamed Ussi rudia

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante nauliza tena swali la nyongeza ni sababu gani zinazosababisha Wizara kutowaajiri Waandishi wa Habari za Mawiyo, wakati wao Waandishi wa Habari za Mawiyo wanafanya kazi za kuelimisha jamii kwa matukio mbali mbali hasa yake matumiko ya papo kwa papo yanayotokea katika Shehiya zetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Tatu swali lake kama ifuatavyo. Kama tulivyosema Habari za Mawiyo ni habari za matukio yanayotokea katika maeneo tofauti na kwa umuhimu wake katika kuelimisha jamii Wizara yetu haiajiri watu maalum ambao watakuwa waanaleta habari hizi.

Wizara yetu inapokea matukio na habari za aina hizo kwa mtu yoyote binafsi, waandishi binafsi na hata waandishi wa vyombo vyetu. Kwa umuhimu wake kwa jamii zetu matukio hayo yanapotokea sisi huwa tunalipa anayewasilisha matokeo ya aina ile, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana lakini pia namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Ni ukweli kwamba watu wa mawio wengi wana kazi zao wengine wako hawajaajiriwa lakini swali langu la kwanza.

a) Hivi mnazichuja vipi habari hizo na anawajibika nani kama habari zitakuwa za uwongo.

b) Kwa muda mrefu ZBC wamekuwa na watangazaji na waandishi wa habari ambao hawajaajiriwa. Juzi juzi tu mmoja wao alifariki dunia Mardadi Amani ambaye sote tulikuwa tunafikiria ameshaajiriwa na ZBC hadi Waziri ukatangaza kifo cha mfanyakazi wako, lakini mfanyakazi yule hajaajirwa je, kukaa

miaka 20 kazini bila ya kuajiriwa haupingani na Sheria za Utumishi wa Umma.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mheshimiwa bado niombe samahani sana swali la kwanza sikuweza kulisikia naomba arejee swali lake samahani sana pana *echo* nyingi sana.

Mhe. Machano Othman Said: Nimesema swali la kwanza katika majibu ya msingi ya Mhe. Waziri amesema Habari za Mawio mtu yoyote mwenye uwezo wa kuzipeleka wao wanazipokea na kuzitangaza na kwa sababu si wafanyakazi wao, ina maana uwajibikaji wao ni mdogo jee habari kama ya uwongo chombo kitachukuwa dhamana ya uwongo ule ulipelekwa na waandishi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, endapo habari zinawasilishwa pale kwenye kituo chetu habari zile huwa tunazitafutia utafiti na ndio maana habari za mawio hazitoki siku ile ile.

Habari za mawio zilizokusanywa jana zinatoka siku ya pili asubuhi lakini taasisi yetu inafanya utafiti wa kina, uchunguzi wa kina na ndio maana kuna kitu kinaitwa *balancing* ya zile *information* tunapopata taarifa upande mmoja, tunabidi tukahakiki upande wa pili. Endapo kwa bahati mbaya Mhe. Naibu Spika ikitokea tumepata taarifa ambayo si ya ukweli taasisi yetu inakuwa ni dhamana lakini vile vile tuna taratibu zetu na sheria zetu kumchukuliwa hatua yule aliyetupa taarifa zilizokuwa sio sahihi.

Lakini kwa swali la pili kuhusiana na yule mfanyakazi ambaye aliajiriwa au alikuwa akifanyia kazi ZBC napenda kuwahakikishia wananchi wote kwamba pamoja na kukuza kidogo lakini yule mfanyakazi hakufika miaka ishirini si vibaya amefika miaka

mingi isiyopungua kumi na tatu, mfanyakazi yule kweli hakuajiriwa napenda nikiri hilo na nikosa kumchukuwa mfanyakazi endapo kuwa humtaki ukaendelea kufanyia kazi bila kuajiriwa.

Lakini kwa tasnia ya habari na hili lieleweke Mhe. Naibu Spika, tasnia ya habari inaweza kuchukua waandishi mbali mbali bila ya ajira. Moja ya chanzo cha habari kuzipata taarifa za habari kutoka kwa watu mbali mbali ambao watakuwa wanaingia mikataba na chombo chetu, si lazima ajiriwe moja kwa moja. Kwa hivyo wale wafanyakazi ambao walikuwa wameingia kwa mikataba walikuwa wanazifanya kazi zile kwa mikataba na suala hili sisi tumeliona uzito wake, kweli ZBC kwa muda mrefu imekuwa na wafanyakazi wengi na bado wapo wafanyakazi wa aina hiyo wenye miaka saba, minane mpaka kuendelea na sisi tunachukua hatua za kuhakikisha kwamba ufanyaji kazi wao uwe wa mikataba kwa njia ya mikataba na wale wanaopaswa kuajiriwa waajiriwe kwa njia ya ajira. Ahsante sana Mheshimiwa.

Nam. 23

Uzalishaji na Usafirishaji wa Mazao ya Viungo vya Vanila na Pilipili Hoho

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:

Muelekeo wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi mwaka 2017/2018 ni kuendeleza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi, ikiwemo Vanila na Pilipili hoho.

a) Je, mipango hiyo imefikia wapi.

b) Ni sehemu gani kumeanzishwa kilimo hicho cha Pilipili hoho na Vanila.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa kilimo cha Pilipili hoho Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa maweni katika maeneo ya Mtende, Matemwe na Makunduchi ambapo Wananchi wametaka kuhakikishiwa soko. Wizara imefanya mazungumzo na Shirika la ZSTC ili wawe wanunuzi wakubwa wa bidhaa hiyo na kwa sasa bei ya kilo moja ni sh 15,000 kwa daraja la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa vanila Wizara imefanya utafiti wa soko la ndani ambapo bei yake ni shs. 55,000 kwa kilo moja. Hata hivyo zao hili linakumbwa na changamoto nyingi ikiwemo hali ya hewa na usarifu wa zao hilo na wizi.

(b) Mhe. Naibu Spika, kilimo cha pilipli hoho na vanila sio kigeni nchini mwetu aidha, wakulima wa Fujoni, Kiboje Kwambani na Kizimbani, hawa wanalima zao la vanila kibiashara pamoja na vishamba vidogovidogo katika Wilaya ya Magharibi "A" ambavyo vinatumika kwa kutembezea Watalii na shamba darasa. Aidha, kwa upande wa kilimo cha Pilipili hoho zinalimwa zaidi katika maeneo ya Matemwe, Pwani Mchangani na Kandwi kwa kibiashara. Ahsante.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba watu walioshajihishwa wengi wao wakulima kutoka Unguja na hawakutajwa hata sehemu moja walioshajihishwa kutoka Pemba na kwa kuwa Jimbo la Kiwani ni sehemu ya maweni sehemu kubwa.

a) Jee, Mhe. Waziri ni lini watu wa Jimbo la Kiwani na wao wanashajihishwa kuhusu kilimo cha pilipili hoho.

b) Hapa ametueleza kwamba daraja la kwanza la pilipili hoho ni Shs. 15,000/= jee daraja jengine ni shilingi ngapi ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kuhusu swali la Kiwani Mhe. Mwakilishi tutakuja na wataalamu wetu tutawaita na wao kuwafahamisha na kuwashajihisha. Lakini vile vile nikukumbushe tu kwamba sasa hivi Pemba zaidi wameelekezea kwenye mikarafuu zaidi, kwa sababu mnamo miaka ya zamani zilikuwa zinalimwa pilipili nyingi kutoka Pemba maeneo ya Mwambe. Lakini tutawaleta wataalamu wetu tuweze kuwapa taaluma hiyo waendelee katika kilimo hiki cha pilipili hoho.

b) Daraja la kwanza nilisema ni shilingi 15,000 na daraja la pili itategemea na ile *quality* yenyewe, lakini kila inavyoendelea kuwa ile daraja kama ni la pili basi inashuka ile bei inaweza ikawa ni 13,000 au 12,000 na kuendelea zaidi. Ahsante.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, swali langu kwa Mhe. Naibu Waziri sasa hivi na wakati huu mtu akiwa nazo pilipili hoho akauze wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kama nimemsikia vizuri anasema mtu mwenye pilipili hoho akauze wapi. Sasa hivi hawa wenyewe *ZSTC* wanazifata pilipili zilipo na wanazinunua. Kwa hiyo, Mheshimiwa ningeomba tu aende *ZSTC* akaseme zitaangaliwa kiwango na ziko vipi kwa sababu nazo zinaangaliwa, basi watamalizana huko huko wenyewe.

Nam. 39

Kufanyika Utafiti wa Maeneo ya Uvuvi

Mhe. Miraji Khamis Mussa – Aliuliza:

Kwa kuwa sehemu kubwa ya uchumi wa Zanzibar inategemea sekta ya uvuvi na katika kukuza matokeo mazuri, wizara inalazimika kutambua maeneo yenye kupatikana samaki kwa wingi (*Fishing Group*) kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara.

(a) Je, ni lini serikali itakuwa tayari kufanya utafiti (*Fishing Group*) na kutambua maeneo yenye samaki wengi kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wa Zanzibar.

(b) Je, serikali haioni kuwa kutokufanya utafiti na kuwaelekeza wavuvi wetu inawakosesha kuongeza kipato ambacho kingewasaidia kuendesha maisha yao vizuri na kukuza pato la Taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inafanya utafiti katika nyanja za uvuvi yakiwemo maeneo ya uvuvi (*fishing ground*), wingi wa rasilimali za samaki na miamba ya matumbawe kwa mfano: (1) (*coral reefs monitoring*), (2) (*frame survey*) na (3) (*potential fishing zone*).

Mhe. Naibu Spika, wizara itawasilisha taarifa hizi kwa wavuvi ikiwa pamoja na matokeo ya tafiti hizo kulingana na eneo husika ili kuimarisha wavuvi kujua maeneo mazuri ya uvuvi. Hatua hii itasaidia kuimarisha sekta ya uvuvi kwa kuwezesha wavuvi kupata tija zaidi kutokana na kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, wizara imeshatayarisha mpango huu wa maendeleo ya uvuvi (*Fisheries Master Plan*), vile vile wizara inaendelea kushirikiana na taasisi za utafiti ikwemo TAFIRI, *IMS* na *SUZA*.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, lakini kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaonesha wazi yataleta faida kwa wavuvi wetu. Lakini naomba kumuuliza swali moja lenye (a) na (b).

a) Ni maeneo yepi yaliyofanyiwa utafiti katika visiwa vya Unguja na Pemba na ambayo matokeo yake yamefikishwa kwa wavuvi husika.

b) Ni mafanikio gani katika maeneo haya yaliyopatikana baada ya kupata matokeo hayo ya utafiti. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Mwakilishi maeneo ambayo tumefanya utafiti bado hatujapeleka ule utafiti kwa sababu upo katika *process* unaendelea kwa kupitia Mradi wa *CO FISH* tunatarajia labda mwakani kukamilisha, kwa sababu mradi huu sasa hivi una miaka lakini mpaka sasa hivi tuna miaka mitatu. Kwa hiyo, baada ya miaka minne kukamilisha kwa mradi huu tutakuwa tumekamilisha hizi tafiti zetu. Lakini mpaka sasa hivi katika maeneo mabayo yameshafanyiwa tafiti ni Nungwi, Fundo na Mtende lakini bado haijapelekwa kwa ajili ya wananchi kutumia.

Mhe. Naibu Spika, na mafanikio yatapatikana mazuri kwa vile bado haijapelekwa siwezi kusema *exactly* mafanikio yamepatikana vipi lakini nategemea mafanikio yatakuwa mazuri na wavuvi wetu watafaidika kuvua samaki hao. Ahsante.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri ameeleza wizara imetayarisha mpango mkuu wa uvuvi. Napenda kuuliza swali moja lenye kipengele (a) na (b).

a) Je, mpango huo mkuu wa maendeleo ya uvuvi umeanza lini na umefikia hatua gani katika utekelezaji wake.

b) Kwa kuwa taasisi hizi za utafiti zinatafautiana kuna uwiano gani katika utendaji wa kazi zao za tafiti. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ningeomba lile swali la pili ndio alirudie.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis lirudie swali lako la pili.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, swali la (b) nimeuliza kwa kuwa taasisi hizi mbili za utafiti zina tofautiana kuna uwiano gani katika utendaji wa kazi zao za tafiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, siruhusiwi kuuliza swali lakini sijui taasisi mbili zipi ambazo amekusudia ili niweze kumjibu kwa ufasaha swali lake.

Mhe. Naibu Spika: Mimi naomba ulijibu kwanza hilo la mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Haya ahsante sana.

Mhe. Mwakilishi nimesema mpango huu wa *Fisheries Master Plan* upo katika hatua ya mwisho, upo kwa Mshauri Elekezi tunasubiri arudishe ili baadae tuangalie na tuweze kuutumia mpango huu. Kwa hatua iliyokuwepo ipo katika Mshauri Elekezi. Ahsante sana.

Mhe. Mwakilishi swali lako la utafiti sijui umekusudia tafiti mbili zipi hizo.

Mhe. Naibu Spika: Tumalize na tunamsubiri Mhe. Mwenyekiti aje kwa ajili ya kuendelea na kikao. Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi nikaweza kupata kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe Naibu Waziri. Kwanza nimpongeze sana kwa majibu yake mazuri, lakini pia ningependa nimuulize ametutajia taasisi tatu ambazo ndizo zinazojishughulisha na haya masuala ya utafiti. Na katika taasisi hizo tatu alitaja taasisi ya TAFIRI, hii Taasisi ya TAFIRI ndio ipi angetuelezea kidogo. Lakini katika hiyo mipango ambayo inaendelea na hizo tafiti hii taasisi ya TAFIRI inajishughulisha na tafiti gani na hii *SUZA* nayo imepangiwa tafiti hizo ifanyie sehemu gani, tungeomba atueleze hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa kutoa ufafanuzi mzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nimesema wizara yangu inashirikiana na taasisi hizi, hizi ni taasisi binafsi kwa hivyo tunashirikiana katika masuala haya ya utafiti wa *fishing ground* na kila kitu ili tuweze kuleta tija kwa wananchi wetu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. TAFIRI ni Taasisi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na mambo ya uvuvi, *SUZA* ni Chuo chetu Kikuu ambacho kina *department* maalum ya *Marine* nayo yenyewe tunashirikiana kwa pamoja kufanya hizi tafiti. Kwa hivyo, ni chuo na taasisi za serikali na zinashirikiana pamoja kufanya huu utafiti

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu wa maswali umemalizika, kwa hivyo tunaendelea na hati za kuwasilisha mezani.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali mbali ya Mwaka 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu kabla ya kuendelea naomba sasa nimpishe Mhe. Mwenyekiti ili aweze kuendelea. Mhe. Mwenyekiti, karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwa heshima kubwa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu Mola wetu kwa kutujaalia kukutana tena leo hii ndani ya ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi tukiwa wazima na tayari kuendelea na majukumu yetu ya kazi.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake imara, makini na thabiti na kwa kazi yake nzuri na ya mfano anayoifanya ya kuweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu na kwa kasi yake kubwa ya kazi anayoendelea kuifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumuombea dua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na familia yake yote Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, ampe umri mrefu, amzidishie hekima na busara ili aendelee kutimiza majukumu yake ya kazi na kuwatumikia Wazanzibari kwa kufuata misingi ya sheria, haki na utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Nawashukuru sana kwa michango yao ya kujenga waliyotoa wakati tulipokutana na kujadili vifungu vya mswada huu. Mengi waliyonishauri nimekubaliana nayo na nachukua fursa hii kuihakikishia kamati ushirikiano wangu na wa afisi yangu ili tuzidi kuisaidia kamati yetu iweze kutimiza majukumu yao ya kazi kwa ufanisi bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unawasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ya baadhi ya vifungu vya sheria zifuatazo.

1. Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam.12 ya Mwaka 1992
2. Sheria ya Mitaji ya Umma Nam.4 ya Mwaka 2002
3. Sheria ya Utumishi wa Umma Nam.2 ya Mwaka 2011
4. Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam.1 ya Mwaka 2017
5. Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar Nam.6 ya Mwaka 2014
6. Sheria ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam.4 ya Mwaka 2015
7. Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali Nam.11 ya Mwaka 2013
8. Sheria ya Makampuni Nam.15 ya Mwaka 2013
9. Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Nam.11 ya Mwaka 2016 na mwisho
10. Sheria ya Mafao ya Viongozi Maalum Nam.5 ya Mwaka 2003.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla mswada huu umegawika katika Sehemu Kuu 11.

Sehemu ya Kwanza, kama ilivyo kawaida inahusu masharti ya awali pamoja na jina fupi la sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili, inahusu marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nam.12 ya Mwaka 1992, katika sehemu hii inapendekezwa kufanya marekebisho ya kifungu cha 3, 46 na 47.

Sehemu ya Tatu, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Mitaji ya Umma Nam.4 ya Mwaka 2002 na inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 8 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) na (3).

Sehemu ya Nne, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam.2 ya Mwaka 2011. Marekebisho katika sehemu hii kimsingi yanahusu kufutwa kwa kifungu cha 15(1) na badala yake kuweka kifungu kidogo kipya cha 15(1).

Sehemu ya Tano, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam.1 ya Mwaka 2017. Kifungu kimoja kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho.

Sehemu ya Sita, inahusu marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba Nam.6 ya Mwaka 2014 na inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 7 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 5 ambacho kinahusu kuzuia kwa Shirika kuuza mali bila ya idhini kutoka Baraza la Mapinduzi.

Sehemu ya Saba, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam.4 ya Mwaka 2015 na inapendekezwa kufanywa marekebisho kwenye kifungu cha 41.

Sehemu ya Nane, inahusu marekebisho ya Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Nam.11 ya Mwaka 2003. Marekebisho katika sehemu hii ni kuongezwa kwa kifungu kipya cha 9(a).

Sehemu ya Tisa, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Makampuni Nam.15 ya Mwaka 2013. Katika sheria hii marekebisho mengi yanayopendekezwa ni kuongeza baadhi ya tafsiri na kuweka vifungu vipya ambavyo vinaweka sawa baadhi ya vifungu ambavyo vilikuwa havisomeki vizuri.

Sehemu ya Kumi, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali ya Serikali Nam.11 ya Mwaka 2016. Marekebisho yanayopendekezwa ni kuongezwa kwa kifungu kipya cha 65(a) mara tu baada ya kifungu cha 65 ambacho kipo sasa kwenye sheria.

Sehemu ya Kumi na Moja, Mhe. Mwenyekiti, inahusu marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Viongozi Nam.5 ya Mwaka 2003. Katika sheria hii marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza kwa kifungu cha 6 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 3 mara baada ya kifungu cha 2.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wauchangie mswada huu na hatimae wapitishe vifungu vyote ambavyo vimependekezwa ndani ya mswada huo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Mwenyekiti, karibu.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hotuba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo katika kutujaalia neema ya afya na uhai iliyotuwezesha kukutana tena hapa leo ili kujadili Mswada huu muhimu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, aidha baada ya kutanguliza shukurani zangu hizo, sasa nitangulize kusema kuwa, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi inakubaliana na marekebisho yaliyofanywa katika Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka Masharti yaliyo bora ndani yake, mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuweka misingi iliyo bora katika mapungufu yaliyomo katika sheria hizo na vile vile kuweka masharti bora ili kwenda sambamba na malengo ya kuwepo kwa sheria husika katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile, nachukua fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na watendaji wake wote wa Afisi yake kwa juhudi kubwa walizozifanya katika kusimamia marekebisho ya sheria hizi.

Hata hivyo, juhudi za afisi hii pekee zisingefanikiwa kama kwamba hawajapata mashirikiano kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo kwa nafasi kubwa ndio msingi na wahusika wakuu wa kufanya marekebisho hayo. Tunawaomba wazidi kutafuta na kuleta marekebisho mbali mbali kwa lengo la kuwezesha sheria zetu kutekelezeka kiurahisi na kuleta haki na usawa kwa kila mmoja miongoni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, napenda kuitumia fursa hii kuwashukuru wadau mbali mbali ambao kamati yetu ilikutana nao kwa mashirikiano yao makubwa yalioonesha na kupelekea kuweza kutoa maoni mbali mbali kwa lengo la kuuboresha Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa kushirikiana na wizara husika pamoja na wadau mbali mbali walioalikwa imeupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu, kuujadili na kushauri mambo mbali mbali kwa mnasaba wa kujenga na kufanikisha matakwa ya Mswada huu wa Sheria, ambapo marekebisho mbali mbali yamependekezwa kufanywa na Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul–latif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe.Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Nd. Haji Jecha Salum	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi kwa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo ya ziada ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo tayari yameshasambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe. Kuna Jadweli la Kwanza na la Pili.

Mhe. Mwenyekiti, katika Sehemu ya Pili ya mswada huu inayohusu Sheria ya Umiliki wa Ardhi, Namba 12 ya 1992, Katika kifungu cha 4 cha mswada, Kamati inashauri kuongezwa maneno yafuatayo mwishoni mwa kifungu kidogo cha (6) kilichoongezwa mara tu baada ya neno "Ardhi"

Maneno yenyewe yatakuwa hivi:

> "Uamuzi wa Rais utakuwa wa mwisho na hautohojiwa na Mahakama yoyote".

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapendekeza kuongezwa kwa maneno hayo ili kuonesha kuwa uamuzi wa mwisho wa haki ya umiliki wa ardhi Zanzibar ni wa Rais na hivyo, haitakuwa vyema kwa taasisi yoyote kuingilia uamuzi ambao umefanywa na Rais hasa tukizingatia kuwa Rais ndiye mmiliki wa ardhi yote ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika Sehemu ya Saba inayohusiana na marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi, Nam. 4 ya 2015, kifungu cha 21 cha mswada huu. Kamati imeshauri kuwa, kifungu cha 41 cha Sheria mama kiwe na kifungu cha 41(1) na kuongeza kifungu kidogo cha (2) kifuatacho:

“(2) Baraza litakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo juu ya taarifa iliyowasilishwa na waziri kutokana na marekebisho yaliyofanyika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 41(1)”.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapendekeza kuongezwa kwa kifungu hiki kwa kuwa marekebisho yaliyopendekezwa katika kifungu cha 41 cha sheria mama hayakutoa fursa na uwezo kwa Baraza la Wawakilishi kutoa baraka zake pindi itakapohitajika katika taarifa itakayowasilishwa na waziri chini ya kifungu cha 41 cha sheria mama.

Mhe. Mwenyekiti, katika Sehemu ya Nane ya Mswada huu inayohusu Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003, ambapo marekebisho yamefanywa kwa kuongeza kifungu cha 9A (Jadweli - Mwenendo wa Bodi).

Kamati inashauri kufutwa kwa kifungu cha 11(1) cha Jadweli hilo na kuandikwa upya ili kuleta muamala mzuri wa kimantiki wa kisarufi kama ifuatavyo:

“(1) Bodi inaweza katika utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati yoyote kufanya kazi maalum kama itakavyoagizwa na Bodi”.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya mapendekezo ya mswada huu yaliyowasilishwa na kamati, vile vile kamati inaomba kuwasilisha mapendekezo yafuatayo, ambayo yameambatanishwa katika jadweli dogo lililotolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kamati inaiomba serikali kuyakubali kwa ajili ya kutekeleza utekelezaji bora wa sheria ya umiliki wa ardhi, Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992, katika Sheria mama ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mapendekezo haya kamati inaishauri serikali kuangalia masharti ya Kifungu cha 56'A' na 'B', kwani masharti hayo yanakwenda kinyume na msingi wa sheria ya ardhi kuwa mali ya serikali na kwa kuzingatia kuwa, Kifungu 24 cha Sheria na Kifungu 23 cha Sheria ya Ardhi kinaweka wazi kuwa, pale serikali itakapotoa ardhi ama kwa utaratibu wa haki ya matumizi ya ardhi au kwa kukodisha haizingatii thamani ya ardhi wakati wa kutoa ardhi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu 63 kinaweka sharti kwa serikali kulipa thamani ya vitu vilivyokuwa juu ya ardhi wakati inapositisha haki ya matumizi ya ardhi au ukodishaji wa ardhi na sio kuzingatia thamani ya ardhi ambayo ni mali ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo, tunaishauri serikali kukifuta kifungu 56 na kukiandika upya kwa kuzingatia misingi iliyotajwa hapo juu kama ilivyoainishwa katika jadweli la marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa marekebisho hayo yataondoa mgongano wa vifungu vilivyopo hivi sasa, lakini pia yataendana sambamba na dhamira na azma ya serikali ya kutoa ardhi bila ya kuzingatia thamani ya ardhi yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia tunaiomba serikali kuyazingatia na kuyafanyia kazi yale yote yaliyopendekezwa na kamati, hata yale ambayo hayakuwa katika mswada huu kwa kushirikiana na wadau mbali mbali na taasisi ambao kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa maoni yao ili kufanikisha sheria hizi zitakapoanza kutumika ziwe na ubora zaidi. Kwa kufanya hivyo, ni kusaidia serikali na taasisi husika kuepuka udhaifu wa sheria zinazofanyiwa marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza haya machache nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wenye hekma na

busara waweze kutumia uweledi wao kuuchangia na kuurekebisha Mswada huu kwa kutoa mawazo yatayosaidia kiutendaji ili kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha mswada huu ili iwe sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. Sasa Waheshimiwa Wajumbe nina majina mawili mpaka sasa na mchangiaji wetu wa mwanzo kwa sasa nimuite Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia machache na mimi juu ya Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbali mbali. Vile vile tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika mikutano hii ya kawaida ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kuweza kuwashukuru na kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na watendaji wake kwa kuweza kuwasilisha mswada huu muhimu wa marekebisho ya sheria mbali mbali. Vile vile kwa hotuba yake nzuri ya ufasaha ya utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nimshukuru na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum na wajumbe wenzake kwa kuweza kuwasilisha ripoti yao inayohusiana na marekebisho ya sheria mbalimbali katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu kwanza nianze na suala zima la umuhimu wa mswada huu. Mheshimiwa nimejaribu kuangalia mswada huu na nimeyaona maeneo manne ambayo ni

muhimu sana, yote ni muhimu, lakini kuna suala zima la uuzaji holela wa majengo ya serikali, ukodishaji wa majengo ya serikali, umilikishaji wa ardhi na maposho na mishahara katika Bodi za Mashirika ya Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba serikali yetu kwa kipindi kikubwa sana naweza kusema kwamba imeumizwa kweli na wenzetu ambao tuliwapa majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la uuzaji wa majengo ya serikali katika Sehemu ya Kumi, ukweli ni kwamba marekebisho ya sheria hii ambayo yamefanywa basi yataipa ahuweni sana serikali yetu katika kipindi hiki. Kwa sababu, Mheshimiwa labda niseme tu kwamba, inawezekana sina uhakika, lakini inawezekana vile vile kwamba serikali haina *asset register* ya majengo yake ya kuyatambua. Hali hii inawezekana kwamba majengo mengi yameuzwa ya serikali kinyume na utaratibu, lakini vyengine inawezekana vile vile kuna majengo yameuzwa bila ya kuzingatia vile vigezo vya tathmini ya majengo.

Kwa hiyo, serikali kwa ufupi imeppoteza rasilimali zake za majengo katika kipindi kirefu. Kwa mfano, katika *flat* za majengo ya maendeleo katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba zimeuzwa. Nyumba za Serikali ukienda Mazizini hapo utasikia hii imeuzwa kauziwa fulani, kauziwa fulani.

Mhe. Mwenyekiti, hii inasikitisha na kama Rais wetu wa mwanzo Mhe. Abeid Amani Karume atakuja leo basi anaweza akatupiga bakora, kutokana na uuzwaji holela wa majengo ambayo serikali iliyajenga kwa maslahi na maendeleo ya wananchi na serikali yake kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, tukija katika Sehemu ya Sita suala la ukodishwaji wa majengo. Tushukuru sana kwamba katika

marekebisho ya sheria hii, iwapo mamlaka inayohusika itataka kukodisha majengo kwa miaka mingi basi idhini hiyo lazima itoke Baraza la Mapinduzi. Niipongeze sana hatua hii ya marekebisho ya sheria hii.

Ni kweli kwmaba majengo mengi ya serikali yanakodishwa kwa muda mrefu na inakuwa katika kodi hizo pengine haina tija kwa serikali, inawezekana thamani ya kodi ambayo inawekwa ni ndogo ukilinganisha na majengo yenyewe. Lakini pengine yanakodishwa kwa miaka mingi zaidi, lakini vile vile kutokana na tija ndogo ambayo serikali inapata ndio maana imeonekana kuna haja sasa ya mamlaka inayohusika basi inapotaka kukodisha majengo kwa muda mrefu basi ipate baraka na idhini ya Baraza la Mapinduzi ili kuweza ku-*control* rasilimali hii muhimu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la umilikaji wa ardhi katika Sehemu ya Pili, ni dhahiri kwamba suala hili hivi sasa kwamba Rais ana uwezo wa kuweza kufuta pengine hati ambayo ilitolewa ya ukodishwaji au ya uuzaji. Hii ni hatua nzuri sana Mhe. Mwenyekiti.

Ni kweli kwamba tuna sera ya uwekezaji, ardhi nyingi zimepewa wawekezaji lakini ardhi hazitumiki kama vile mikataba ambavyo iliwekwa, kiasi ya kwamba serikali imekosa mapato. Hata hivi sasa niipongeze sana Bodi ya Mapato kwa kuweza kufuatilia ardhi ambazo zimekaa muda mrefu ambazo tumewapa wawekezaji na ardhi zile hazileti tija kwa serikali.

Kwa hiyo, kuwepo kwa marekebisho ya sheria hii juu ya umilikaji wa ardhi itatusaidia sana, serikali kuweza kudhibiti rasilimali yake ya ardhi na pale ambapo itakuwa inatumika basi iwe inaleta tija kwa serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tukielekea katika masuala mazima ya mishahara, maposho katika Bodi za Serikali na Mashirika katika Sehemu ya Tatu, uwepo wa mabadiliko au marekebisho ya sheria hii, basi hivi sasa kutakuwa na uwiyano. Kutakuwa na uwiyano wa maposho katika bodi mbali mbali za Mashirika ya Serikali ili kuweza kuona kwamba serikali inanufaika. Hali ilivyo sasa inawezekana kwamba kuna bodi zina maposho makubwa zaidi kuliko ya bodi nyengine, au mishahara bodi zinaidhinisha mishahara mikubwa zaidi katika mashirika kuliko mashirika mengine. Sasa hali hii kwa hivi sasa kwamba Baraza la Mapinduzi litakuwa ndilo lenye uwezo wa kutoa idhini juu ya uwiyano huu pengine maposho au mishahara basi itaisaidia sana serikali katika kudhibiti rasilimali yake ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli kwamba tumechelewa katika kufanya marekebisho ya sheria hizi, kwa sababu serikali kwa ufupi imeumizwa sana katika maeneo hayo. Ningeomba sana kama itawezekana basi serikali iunde tume kuweza kuchunguza mikataba ambayo haina tija ya ukodishwaji wa ardhi zote ambazo hazitumiki. Lakini vile vile iundwe tume ya kuweza kuhakikisha na kuweza kuipitia mikataba inayohusiana na majengo ambayo yamekodishwa pengine kwa muda mrefu, ili kuweza kuona kwamba serikali inapata tija kutokana na rasilimali yake ya majengo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika marekebisho madogo madogo ndani ya mswada huu nakuja katika ukurasa wa 220 katika Jadweli la Mwenendo wa Bodi, kifungu cha 2(3) mstari wa tatu baina ya neno 'saini' na neno 'wajumbe'. Napendekeza liwepo neno 'na' ili lisomeke yaliyowekwa saini na wajumbe.

Vile vile katika kifungu cha 4 ukurasa huo huo mstari wa tatu, kuna neno ambalo linasomeka, 'atakaeteluliwa' na badala yake lisomeke 'atakaeteuliwa'.

Mhe. Mwenyekiti, tukija ukurasa wa 222 katika kifungu cha 14 naomba nikikariri.

Kifungu cha 14 cha mswada kinasema kwamba:

"Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kwa kiwango atakachoamua waziri baada ya kushauriana na waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha".

Ningependekeza kwamba yamalizie maneno yafuatayo:

" Atakavyoidhinisha muda hadi muda kama katika maeneo mengi ya vipengele hivi yanavyosomeka".

Lakini katika ukurasa wa 223 Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 26 kifungu kidogo cha (ii) mstari wa pili. Naomba nikariri itakayojulikana kama kampuni binafsi ya Mjumbe mmoja. ningependa hilo neno Mjumbe liondoke likae, binafsi ya mtu mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 226 sehemu ya 11 katika *title* hiyo kuna neno viongozi ambalo kwa lilivyokaa linasomeka "vioangozi", kwa hiyo isomeke viongozi.

Baada ya marekebisho hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii ya kufungua dimba katika mjadala wa miswada hii ambayo inawasilishwa katika Baraza letu tukufu na niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuweze kupitia na kuichangia na hatimae tuweze kuupitisha mswada huu muhimu katika marekebisho ya sheria mbali mbali za serikali.

Baada ya hapo nikushukuru na naunga mkono hoja hii au mswada huu wa marekebisho ya sheria mbali mbali asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Makame Rashid Shamsi wa Jimbo la Magomeni kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Shihata na atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na mimi kutoa mchango wangu juu ya marekebisho ya Sheria mbali mbali ili tuweke mambo sawa katika utekelezaji wake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali Mhe. Rais na Baraza la Mapinduzi kwa kuona umefika wakati sheria zote ambazo zina kasoro zifanyiwe marekebisho ili kuleta ufanisi katika wakati tuliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, tuna sheria kumi hapa.

- Sheria ya Umiliki wa Ardhi namba 12 ya mwaka 1992
- Sheria ya Mitaji ya Umma namba 4 ya mwaka 2002
- Sheria na Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011
- Sheria ya Uchaguzi namba 1 ya mwaka 2017
- Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar namba 6 ya mwaka 2014
- Sheria ya Tume ya Maadili ya Viongozi ya Umma namba 4 ya mwaka 2015
- Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na namba 11 ya mwaka 2003
- Sheria ya Makampuni ya mwaka 2013, Sheria ya ununuzi ya Uondoaji wa Mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016

- Sheria ya Mafao ya Viongozi Maalum namba 5 ya mwaka 2003.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kama nilivyosema kwa kuzingatia haya umefika wakati kwamba yaangaliwe na yazingatiwe ili yapate ufafanuzi mzuri na utendaji.

Lakini pili nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa dhati kabisa kwa kukaa na wenzake na kuona kwamba sheria hizi zifanyiwe marekebisho ili zilete maendeleo katika nchi yetu.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba sheria hizi zote muhimu na zimekuja wakati unaofaa. Nitakuwa na machache ya kuchangia baadhi ya sehemu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho ya sheria sehemu ya pili, Marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi namba 12 ya mwaka 1992. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi ya Zanzibar kero lao kubwa katika mambo mbali mbali hasa baada ya kuja utalii katika nchi yetu ardhi imekuwa ni mali na kwa bahati mbaya ardhi yenyewe kwa Zanzibar haipo. Lakini hapo zamani kulikuwa hakuna utata wa ardhi kwa sababu wananchi wengi wanaoishi vijijini hasa ukanda wa mashariki au kaskazini mashariki pwani na kusini walikuwa hawana ugomvi wa ardhi kwa sababu ardhi yote ilikuwa iko sehemu za pwani huku, lakini mara baada ya kuja utalii ardhi imekuwa changamoto kubwa na inaleta ugomvi mkubwa kwa wananchi. Aliyekuwa mtu ambaye hashiriki au hakai katika maeneo hayo atadai eneo hili ni langu kwa maslahi yake juu ya kutafuta fedha kwa kujiendeleza maisha yake.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba sheria hii naipongeza na kwa kusema tu kwamba hivi sasa hivi inasimamiwa vizuri na itakuwa na mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba tunaifanyia kazi ipasavyo na kuondoa kasoro zilizokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho hayo ya kifungu cha 3 kinasema kwamba kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (ii) na (iii) Rais akiridhika na ushahidi uliopelekwa mbele yake atafute uamuzi uliotolewa na Waziri unaohusiana na ugawaji wa ardhi. Maana yake nimeifahamu vizuri tu kwamba kitu chochote katika nchi yetu hasa sehemu ya ardhi, ardhi mwenye mamlaka mwisho ni Rais na Ardhi hiyo bila ya yeye itakuwa na malalamiko mengi na ugomvi mwingi sana kwa sababu baadhi ya wanyonge huenda wakakosa haki zao kwa kuachiwa mtu ambaye siku nyengine kidogo atatetemeka.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba hili ni zuri na naipongeza sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuliangalia hili na kuliona kwamba linafaa. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo litatupa manufaa sana kwa wananchi wetu hasa wanyonge.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, mkataba wa ukodishwaji wa Ardhi ya Umma iliyotolewa chini ya masharti ya kifungu cha 4 cha kifungu hichi utafutwa mara baada ya kufutwa kusitishwa kibali cha uwekezaji. Hii pia tafsiri yake ni nzuri kwa sababu uwekezaji katika mkataba wetu wa ardhi uliokodishwa utamalizika pale kibali cha muwekezaji kitakapomalizika. Lakini pia ataongezewa kibali hicho ikibidi uwezekano huo una manufaa katika kueleta maendeleo katika nchi yetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6 cha 47(i) Sheria Mama inafutwa na kuwekwa kifungu kipya cha kwanza (i) na (ii) ifuatavyo:-

(i) Mkataba wa ukodishwaji wa Ardhi ya Umma iliyotolewa chini ya masharti, sehemu hii hautazaidi miaka 99.

Maana yake nimeifahamu vizuri. Mheshimiwa kuna watu wengi tunashituka na wanashituka wengi tu kuambiwa ardhi

imekodishwa kwa miaka 99 huu ni mshituko. Lakini kumbe tafsiri yake sasa hivi imekuja vizuri katika marekebisho itakwenda kwa awamu kila miaka 33 itakaa tena na kufanyiwa utaratibu ambao unafaa kwa kuleta maendeleo katika jamii yetu ambayo inahusika. Kwa hivyo, na hili nalipongeza ni zuri na linaleta ufanisi katika utendaji wa kazi zetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, suala la bodi zetu. Bodi zetu tumeelezwa tu katika mambo mbali mbali kuna mambo ya kukaa pamoja na kutafakari kwa sababu kuna bodi kubwa na bodi ndogo, lakini jina la bodi zote sawa sawa.

Kwa hivyo, na hapa kutakuwa na uwiano kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mambo ya serikali yanakwenda katika moja na umoja wenyewe kama kitawekwa kipengele fulani bodi iwe kiasi fulani basi itakuwa kwa bodi zote.

Mimi naipongeza sana serikali kwa kuliona hili kwa sababu suala kubwa linaloleta utata katika maeneo mbali mbali ni manun'guniko kwa baadhi ya bodi ambazo tunazo huwa nasikitika kwamba mapato yao hawa madogo au yanakuwa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla msaada huu nimesema tu kwamba una marekebisho niliyoyataja 10. Lakini tuseme tu kwamba marekebisho hayo ni ya utendaji na baada ya kuyasoma Mwanasheria na marekebisho ya Kamati yetu ya Katiba , Sheria na Utawala Bora Mwenyekiti wake kaisoma vizuri na kafafanua mambo mazuri ya kuleta marekebisho ambayo kwa manufaa ya kuleta maendeleo katika kuyapanga hayo yaliyotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maadili ya viongozi ni suala zuri, lakini pia suala hili kama nilivyosema sheria inafanyiwa marekebisho na mambo mengineyo ambayo ya kutengenezwa ili liende vizuri. Mara nyingi wahusika katika suala hili viongozi

wengi wanakuwa wanababaika au wanakuwa hawajiaelewi wakati mwengine kwa sababu utakuta katika maelekezo moja, mbili, tatu lakini baada ya kupata sheria hii na marekebisho mazuri basi kila mtu atajifahamu wajibu wake na kuondoa kasoro ambazo zimejitokeza huko nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba sina mengi sana katika sheria hii hasa tukizingatia kwamba haya ni marekisho ambayo yana tija katika kuleta ufanisi katika kazi zetu. Kwa hiyo, niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele naipongeza tena serikali naipitisha au nimeikubali mswada huu kwa asilimia mia moja sina matatizo nao. Nashukuru ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie machache katika mswada huu ulioko mbele yetu.

Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu na namuomba aniwezeshe nisimame hapa nitoe mchango wangu alau mchache ulipo katika mswada huu.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, sina budi niipongeze Serikali ya Mapinduzi za Zanzibar ikiongozwa na Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein kwa kukubali kuletwa msaada huu mbele yetu ambao kuwa ni muhimu sana kwa nchi yetu, mswada ambao kuwa umebeba mambo mengi sana kama alivyotaja Mhe. Mjumbe alietangulia hapa. Lakini na mimi nikaona sina budi na mimi lazima nitoe ahsante yangu na shukurani wakishirikiana pia na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Watendaji wake kwa kazi kubwa waliona kwamba hapa na hapa tufanye nini. Kwa hivyo, wale wote tunawapongeza sana.

Lakini pia kwa Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum ambao kuwa wameupitia mswaada huu na kuona kwamba vipengele mbali mbali kwa upana kabisa wakaanza kuvileta, hata mimi mwenyewe nilikuwa nivitaje hivyo lakini baada ya kuona waraka wao huu wa marekebisho na mimi nimeviondoa vifungu vile kwa kuokoa muda nikaona nisivitumie tena vile kwa vile tayari vimeshafika mbele yetu.

Lakini hata hivyo kwa muono wangu kuna mawili matatu nimeyaona katika sehemu ya mswada sehemu ya pili ya marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi namba 12 ya mwaka 1992.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchangio wangu mimi kifungu namba 6 kinachosema marekebisho ya kifungu 47 ya sheria mama kifutwa na kuweka kifungu kipya cha (i) na (ii) kama ifuatavyo:-

Mkataba wa ukodishwaji wa Ardhi ya Umma uliotolewa dhidi ya masharti ya sehemu hii hautazidi miaka 99 ambayo itatolewa kwa utaratibu wa awamu wa miaka 33 kwa kila kipindi. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa bado nalalamikia kama wanavyolalamika wananchi wenzangu huko kwamba miaka 99 kwamba hii ilikuwa ni miaka mingi sana. Hapa ni sawa sawa na kuiuza nchi.

Kwa hivyo, kuona hapa kwamba hii haki yetu ya ardhi hii inalindwa na inaleta faida kwa wote baada ya kuoneshwa familia moja kwa mtu mmoja wanarithishana basi naona huu muda upunguzwe sana. Kama hapa imeoneshwa 99 mimi nasema miaka iwe 30 itoshe kwa ukodishwaji wa ardhi hii na hiyo miaka 30 kila baada ya miaka 10 ndio aweze kuangaliwa tena mtu ameitumia vipi ardhi hii.

Hiyo miaka 33 bado ni mingi kuona kwamba ndio ianze kutizamwa amefanya nini, ukitizama mimi hapa nilipo nimeitumia

ya serikali miaka 35. Sasa na leo ukitizima kwamba muwekezaji apewe miaka 33 ndio anakuja kuangalia je, vipi ardhi ameitumia ni muda mwingi sana. Mimi mwenyewe nimetumia miaka 35 toka nalipwa silingi kumi hadi leo nalipwa kama ivyo ilivyo. Lakini hii sheria kwa hapa tuirekebishwe iwe miaka 30 na kila baada ya miaka 10 ndio iangaliwe imeendelezwa vipi. Huo ni mchango wangu naomba marekebisho hayo kama yatazingatiwa yafanyike.

Lakini jengine sehemu ya 3 Marekebisho ya Sheria ya Mitaji ya Umma. Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 7 Marekebisho ya Sheria ya Mitaji ya Umma namba 4 ya mwaka 2002 kifungu namba 7 ya mswada huu sehemu hii itasomwa pamoja na sheria ya Mitaji ya Umma namba 4 ya mwaka 2002 ambayo katika sehemu itajulikana kama sheria mama.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria hiyo ya Mitaji ya Umma wenzetu wanaitumia vibaya wakati mwengine. Utatuzi wa ardhi leo au muwekezaji anapewa sehemu matokeo yake wanaondoka kimya kimya wanakabidhiana wanapeana kinyemela nyemela kwa kutumia jina lile lile lakini muwekezaji yule ni mwengine.

Kwa hivyo, wawekezaji wa aina hii waangaliwe kila baada ya muda kwenye mitaji yao hii ya umma iliyopo hapo iangaliwe kila baada ya muda tuone kwamba itafanya vipi na itaweza vipi kusaidia serikali yetu hii. Jambo hili ni muhimu sana kuzipitia nyaraka ambazo zinahusiana na mambo haya ya Mitaji ya Umma hapa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni pale ambapo kuwa kamati imeona vipengele mbali mbali ikiwemo lugha na mimi sitaki nivirejee nimeona kwamba baada ya kupitia waraka huu nimeridhika nao sana Mswada huu wa sheria ulioletwa mbele yetu nasema kwamba naunga mkono mia juu ya mia na naipongeza sana

serikali kutuletea mbele yetu hii na naomba sana Mhe. Rais na wewe aungalie kwa haraka ili uweze kufanya kazi.

Lakini basi pamoja na sheria hii tuliyoileta tunaijadili nimuombe Mwanasheria na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba kuna sheria ambazo tumeshazipitisha hapa na zinaanza kufanya kazi lakini bado zinalalamikiwa na wananchi wetu kwamba zinaleta athari. Kama vile ambavyo tumeona kwamba sheria zilizomo humu tufanye marekebisho basi na hiyo tuifanyie marekebisho, ziko kama vile Sheria ya Pencheni ambayo kuwa tumeshaipisha hivi karibuni kwa kweli inalalamikiwa na wananchi na hivyo kuna haja ya kuletwa mbele yetu hapa tuiangalie tena upya.

Kwa hivyo, lengo la kutunga sheria iweze kutusaidia sote na vizazi vinavyokuja. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda huu ulionipa. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kama walivyotangulia wenzangu naomba nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache sana katika mswada huu wa marekebisho ya sheria mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nashukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuona umuhimu wa baadhi ya changamoto zinazogusa katika taasisi zetu mbali mbali ambazo wakati mwengine zinasababisha utendaji wa kazi kuweza kusuasua na kuweza kutuletea kwa ajili ya kuweza kufanya marekebisho madogo madogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa nataka nianze kutoa maoni kidogo kabla sijaingia katika huu mswada wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu ajaribu kuziangalia na sheria zinazohusu makosa ya barabarani na vyombo vya moto vile vile kwa sababu kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati sana. Kuna baadhi ya adhabu nyengine tokea wakati wa Mkoloni. Kwa hiyo, inafika pahala hawa watumiaji wa vyombo vya moto wakati mwengine mtu haoni tabu yeye kufanya kosa akapelekwa Mahakamani akatoleshwa faini ambayo pengine haizidi shilingi elfu kumi.

Kwa hiyo, kitu yeye anaona aah! hiki *just simple*. Kwa hiyo, naomba ofisi yake pamoja na jitihada ilizozifanya kwa ajili ya kuleta marekebisho ya baadhi ya sheria, pia wangelijaribu kuangalia na hizi sheria za barabarani zinazohusiana na vyombo vya moto. Kwa sababu mara nyingi tumekuta *traffic* wanakuwa wanalalamika wanasema kwamba hawa hata ukiwapeleka mtu haoni tabu, anajua akenda pale analipishwa faini ambayo kwake yeye sio *issue*. Kwa hiyo, hili pia nilikuwa naomba ofisi yake Mhe. Mwanasheria Mkuu aweze kulifanyia kazi baadae anapoleta sheria nyengine ndogo ndogo na hizi ziwe zimeshaangaliwa.

Jengine nilikuwa naangalia katika huu mswada kifungu cha 3, sehemu ya pili ya Marekebisho ya Sheria ya Umiliki wa Ardhi, ya mwaka 1992. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sheria zetu za ardhi hapa Zanzibar nafikiri zipo nyingi sana. Kila inapoonekana changamoto inafanyiwa marekebisho inakuja nyengine lakini bado unakuta migogoro ya ardhi inaendelea kutuandama.

Sasa hivi kuna tatizo moja ambalo linagusa zaidi kwa wale watu ambao walikuwa na nia njema kwa wenye mashamba kwamba mtu alikuwa pengine mfanyakazi wake baadae pale akamuachia akajenga kibanda. Lakini sheria inasema kwamba baada ya miaka 12 mtu baada ya kuweka jengo au baada ya kujenga katika eneo

na hakuna malalamiko yoyote yaliyopelekwa ina maana ile nyumba pale umiliki wake unakuwa tayari ni halali. Sasa utakuta kuna watu wamejenga ndani ya mashamba ya watu lakini kwa kuwa imezidi miaka 12 hakuna malalamiko yoyote. Sasa yule mtu anapotaka kuendeleza lile eneo lake, yule anapomwambia ahame watu wanabuburushana kwenye vyombo vya sheria. Akenda kule hakimu anamwambia bwana mpaka sasa hivi huyu mtu yupo zaidi ya miaka 12 kwa hiyo kwa mujibu wa sheria huwezi kumuondoa.

Sasa maeneo kama hayo yapo mengi sana katika maeneo yetu mbali mbali. Nilikuwa naomba bado wataalam wake waendelee kuziangalia hizi sheria zetu za ardhi kwa sababu bado zinaendelea kuwakwaza wananchi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna suala ambalo tunatunga sheria na kama hivi tunarekebisha sheria, lakini bado inarudi pale pale tatizo letu katika utekelezaji wa zile sheria zenyewe. Mhe. Mwenyekiti, sisi ukiangalia sheria zetu za ardhi hasa unapokuja katika maeneo ya uwekezaji, serikali imetoa *lease* kwa wawekezaji mbali mbali. Sheria inasema wazi wazi ndani ya miaka mitatu kama mtu hajaendeleza lile eneo basi lile eneo linakuwa tayari linarudi serikalini.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa ushahidi usio na shaka tayari kuna *lease* nyingi ambazo nyengine hata hazilipwi kodi serikalini zipo zaidi ya miaka 15 maeneo yale hayajaendelezwa na wengine utakuta wamezungusha ukuta tu halafu ndani hamna kitu. Wakati wanakuja wawekezaji wanahitaji kuwekeza katika ardhi zile wanashindwa wanarudishwa hakuna maeneo. Pia kuna wananchi wengine wao wamechukua maeneo wamepewa *lease*, wao wamegeuka kama madalali. Sasa Mhe. Mwenyekiti, utakuta wanakuja wawekezaji mtu anauziwa ardhi inafika mpaka kwenye dola laki tatu, wakati ile kodi ya ardhi pengine kila mwaka labda

analipa dola elfu nne au elfu tano, lakini sasa ardhi zile zinauzwa kwa pesa nyingi sana.

Sasa tatizo linabakia vipi, wale wawekezaji waliokuja wanashindwa kununua bei ile kwa sababu walivyoangalia sera zetu wanaambiwa kule au sera zinasema ardhi ni mali ya serikali. Mwekezaji anakuja anategemea mimi nikenda serikalini, nikenda Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, nikenda *ZIPA*, ina maana kule mimi nitapewa masharti ya serikali. Lakini wawekezaji wetu wanapokuja wanaambiwa waende wakaonane na wananchi kwa ajili ya kuweza kununua ile ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa unamkuta mwekezaji ile *capital* ya kuanzisha mradi inabidi sasa anarudi anakwenda kuinunua ile ardhi. Mhe. Mwenyekiti, wanafika wawekezaji wanatuuliza kwamba hii ardhi ni mali ya serikali au ardhi ni mali ya watu. Sasa hapa lazima tujue kipi na kipi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa serikali yetu inakosa mapato mengi sana, tunakosa wawekezaji wengi sana, wanakuja na mitaji yao, wanakuja na miradi yao lakini kwa kuwa ardhi hakuna wanahangaika wanaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu naomba kwa sababu hii sheria sisemi ije tena, kwa sababu sheria tayari ipo. Kitu kikubwa na kwa bahati Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira hapa simuoni, lakini kupitia marekebisho ya sheria hii nadhani *hansard* imuwezeshe aweze kuangalia zile sheria za ardhi maeneo ambayo yametelekezwa kwa muda mrefu yarudi serikalini, ili sasa serikali iweze kuwatafuta wawekezaji waliokuwa makini kwa ajili ya kuendeleza maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna baadhi ya watu wengine wamepewa *lease* na kwa bahati mbaya sana hizi *lease* kipindi cha

nyuma zilipokuwa zinatoka zilikuwa hazifuati hasa yale masharti ya *lease* inavyotaka. Kwa sababu sheria ya kupewa *lease* mtu anatakiwa aandike mradi wake, andiko lake la mradi apeleke *ZIPA*. Kule kuna kama *One Stop Centre*, kuna watu wa Mazingira, kuna watu wa Ardhi, kuna watu nafikiri mpaka Afisi ya Mwanasheria Mkuu kama sikosei, yaani taasisi zote zinazohusiana na masuala ya ardhi wanakuwepo katika ile bodi ya *ZIPA*. Matokeo yake kuna watu wamepewa *lease* hawana hata andiko la mradi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kupitia hichi kifungu cha 4 na kifungu cha 5 ambacho kinakuja katika marekebisho haya ambapo maeneo haya yanaweza yakarudi serikalini na Mhe. Rais akaweza kuyatolea maelekezo mapya katika suala zima la uwekezaji.

Nafikiri hapa serikali itakuwa imefanya jambo la maana sana. Kama tulivyosema sasa hivi kama kuna mtu ana *lease* lazima *lease* yake ihakikiwe na kwa bahati nzuri sasa hivi Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imo katika kufanya uhakiki na utoaji mpya wa *lease*. Kwa hiyo, naomba sana kabla zile *lease* mpya hazijatoka yaangaliwe sasa yale masharti, kwa sababu hizi *lease* wakati mwengine tulikuwa tunapeana tu kimjomba mjomba, kishangazi shangazi, kindugu ndugu, kirafiki rafiki, mtu hana mradi lakini anapewa *lease*, wakati watu wana miradi *lease* wanakosa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili nilikuwa naomba sana serikali yetu iweze kulisimamia. Kwa sababu kuna watu sio kama hawawezi kuwekeza lakini anahisi kwamba nikiingiza fedha nitatumia pesa zangu faida itakawia kurudi. Lakini eneo hili nikiliuza nitaweza kupata faida zaidi pesa zangu nitaongezea nikatafute mradi mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kupitia hizi sheria zetu kwamba tunashindwa kuzisimamia vizuri, kuna watu wanakuja wanachukua *lease* wanakwenda kutafuta wawekezaji ina maana wao sasa ndio wanapata *capital* ya kwenda kuwekeza katika maeneo mengine.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ile nia na dhamira ya serikali kutoa *lease* kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, vile vile kuongeza ajira inakuwa inakosekana ardhi zinakaa kwa muda mrefu. Sasa hili nilikuwa naliomba sana Mhe. Mwenyekiti, halina haja ya marekebisho ya sheria lakini nakazia tu kwamba sheria iweze kusimamiwa vizuri ili yaweze kurudi serikalini na serikali itafute wawekezaji makini kwa ajili ya kuyaendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4 ambacho kinafanyiwa marekebisho wanasema kifungu cha 3 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo: Naomba ninukuu.

"(6) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), Rais akiridhika na ushahidi uliopelekwa mbele yake atafuta uamuzi uliotolewa na Waziri unaohusiana na ugawaji wa ardhi."

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili pia naendelea kulitilia mkazo. Kwa sababu nilijaribu kufuatilia hii ziara ambayo anaifanya sasa hivi Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini na Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo mwekezaji kapewa *lease*, lakini katika hilo eneo hailingani hicho alichokiwekeza katika eneo hilo na wananchi wamelalamikia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu serikali kuna maeneo tayari imeshayatangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Mfano, eneo hili ni la utalii, ina maana kama eneo la utalii ukenda ukaweka biashara ya kiwanda au uwekezaji wa kiwanda, ina maana

uwekezaji huo sio halali. Sasa maeneo haya ndio ambayo yanatakiwa Mhe. Rais apelekewe aridhie kama eneo ni la utalii basi uwekezaji wake ni wa utalii, kama eneo la viwanda basi uwekezaji wake uwe wa viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia ziara ile ya Mhe. Mkuu wa Mkoa, tuliona kwamba Mkuu wa Mkoa alitoa agizo kuna *lease* alisema kwamba kwanza isitishwe mpaka ajiridhishe na ule mradi ambao unaotaka kufanyika. Kwa sababu ni suala ambalo liko linashughulikiwa sitaki nimtaje mwekezaji wa aina gani na mradi wake ni wa aina gani, lakini nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu akihitaji baadae naweza nikamfahamisha uwekezaji huo uko eneo gani.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kifungu cha 5, kifungu cha 46 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"Mkataba wa ukodishwaji wa ardhi ya umma iliyotolewa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, utafutwa mara baada ya kufutwa kwa kusitishwa kibali cha uwekezaji."

Halafu kifungu kidogo, kifungu cha 6 ambacho nilichokusudia kujenga hoja yangu cha sheria mama kinasema kwamba:

Kifungu cha 47 (1) cha sheria mama kinafutwa na kuweka kifungu kipya cha (1) na (2) vifuatavyo:

"Mkataba wa ukodishwaji wa ardhi ya umma uliotolewa chini ya masharti ya sehemu hii hautazidi miaka tisini na tisa ambayo itatolewa kwa utaratibu wa awamu kwa miaka isiyozidi thelathini na tatu kwa kila kipindi."

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo pia nilikuwa na maneno. Sina uhakika wa visiwa vyetu ukodishwaji wake uko vipi. Lakini *hearsay* inasema kwamba katika maeneo yale na hili labda Mhe. Mwanasheria Mkuu baadae akija anaweza akatusaidia ufafanuzi kwamba wananchi wanasema vimekodishwa miaka 99. Haya marekebisho ya sheria mimi nayakubali sana kwamba hiyo miaka 99 kwa mwekezaji makini wala sio tatizo, kwa sababu kitu kikubwa inatakiwa mradi u-*exist* lakini mradi uwe unafanya kazi na unaleta tija kwa serikali. Lakini kila baada ya miaka 33 ule mkataba utakuwa unapitiwa tena.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tujaribu kuangalia mikataba katika visiwa vyetu. Kwa sababu ukiangalia uwekezaji uliowekezwa katika visiwa hivi haulingani na thamani ya visiwa vyenyewe. Mhe. Mwenyekiti, katika nchi ambayo imewekeza au inategemea zaidi utalii, tulitegemea katika maeneo ya visiwa ndio kuwe kuna uwekezaji ambao utaingiza mapato mengi sana ndani ya serikali. Lakini leo ukiangalia katika visiwa vyetu nakusudia visiwa vidogo vidogo uwekezaji uliowekezwa hauna hasa thamani ya ile ardhi ambayo iliyowekezwa.

Sasa nilikuwa naomba wataalam wetu wachumi wajaribu kuangalia miradi iliyowekezwa katika visiwa vile na thamani ya nchi. Kwa sababu ukisikia Zanzibar, Zanzibar peke yake jina linajiuza. Ukiangalia kwa sababu kuna baadhi tumeshawahi kukaa na *private sector* hawa ambao ni ma-*investor.* Wanasema kwamba katika maeneo ya visiwa duniani ndio kuna uwekezaji ambao wale watu wanaojua kutumia pesa zao kule ndio wanakokwenda ku-*spend* pesa zao. Lakini matokeo yake leo unakwenda unakuta ni vibanda ambavyo havina hadhi hasa ya uwekezaji katika vile visiwa. Maeneo ambayo tunategemea serikali ingeliweza kuongeza mapato makubwa sana.

Kwa hivyo hapa Mhe. Mwenyekiti, hiya marekebisho ya sheria mimi nayaunga mkono, lakini vile vile kuyaunga mkono kwangu basi tuanze kufanya *research* na tuanze kufanya *study*. Je, uwekezaji katika visiwa vyetu umeekezwa katika miaka mingapi? Kama ndio hii miaka 99 basi tuangalie aina ya ule uwekezaji wake na thamani ya ule mradi husika.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa, maana yake naona ushakuwa unanitizama tizama. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nakuja katika ukurasa wa 226 wa mswada wetu Sehemu ya Kumi ya Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika shughuli zetu za *oversight* tunapokwenda kuikagua serikali katika utendaji wa shughuli zao mbali mbali, lakini vile vile katika maeneo mbali mbali. Tumegundua hii sheria ya manunuzi kuna baadhi ya sekta kidogo inakwaza.

Kwa mfano, ukiangalia tuliwahi kutembelea kwenye Bohari yetu Kuu ya Madawa. Katika Bohari Kuu ya Madawa kwamba madawa wanayonunua inabidi yale yanatokana na *requisition* kutoka katika hospitali zetu mbali mbali. Sasa kuna *requisition* nyengine inakuwa ni kubwa, kwa hivyo katika suala zima la utoaji wa tenda linakuwa halina matatizo kwa sababu ni fedha nyingi inayotumika. Lakini ukiangalia kuna baadhi ya *requisition* mahitaji yake yanakuwa ni madogo sana. Sasa ile gharama ya kuitisha tenda lakini vile vile kile kitu au zile *re-agent* zinazotaka kununuliwa zinakuwa ni fedha chache sana.

Mhe Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu ukiangalia katika kifungu cha 108 cha Sheria ya Manunuzi basi kinakwaza kidogo katika shughuli Bohari Kuu katika ununuzi wa baadhi ya madawa pamoja na *re-agent.*

Sasa nilikuwa nashauri kuna baadhi ya maeneo hasa ambayo manunuzi yake hayahitaji pesa nyingi, basi yale masharti ya kuitisha tenda, kwa sababu inaweza kuwa kwa mwaka mzima inawezekana pengine yale manunuzi yasizidi hata milioni 50 kwa mwaka mzima na manunuzi yenyewe yanakuja kwa kila *quarter*. Sasa leo kitu cha milioni 15 ukaitishe tenda kwa kweli kidogo inaleta ukakasi. Suala hili tuliliona na linasababisha hata ununuzi wa baadhi ya *re-agent* wakati mwengine unachelewa kutokana na hii sheria ya manunuzi. Sasa hili pia nilisema nijaribu kulizungumza hapa ili Mhe. Mwanasheria Mkuu baadae aje aangalie hizi sheria na wale wenzetu waweze kufanya *procurement* kwa utulivu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana, namshukuru sana swahibu wangu Mhe. Mwanasheria Mkuu na timu yake kwa kuweza kutuletea sheria hii na naunga mkono kwa asilimia mia moja. Vile vile wajitahidi katika usimamizi wa utekelezaji wa sheria hizi katika maeneo mbali mbali. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye mswada huu wa marekebisho ya sheria mbali mbali. Nianze kusema kwamba mswada huu ni mzuri, ni mzuri kwa maana ya kwamba unalenga kutatua zile changamoto zilizopo katika sera zetu za sasa na hasa kwa upande wa ardhi. Nitoe mfano huko ambako Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu wengi wamelielezea na kutoa mifano mbali mbali.
Lakini pia nikiri kwamba ni kweli tuna changamoto hii kwenye upande wa ardhi. Lakini jitihada zinaendelea za kuhakikisha tunafuata sheria katika kufuta yale maeneo ambayo yanastahiki kufutwa.

Lakini nimesema mswada huu ni mzuri kwa sababu umekuwa ni muarubaini. Ukiangalia kifungu cha 46 iliyopendekezwa kifungu kidogo cha 5 kinaeleza kwamba mkataba wa ukodishwaji wa ardhi wa umma, uliotolewa chini ya masharti ya kifungu (4) cha kifungu hiki utafutwa mara baada ya kufutwa au kufutwa kibali cha uwekezaji. Ina maana sasa itakuwa nafuu.

Kwanza hapa tutakuwa tuna-*save* muda, hatutakuwa tunachelewesha muda tena, sheria yetu ya sasa maana yake uwekezaji kibali chake au leseni yake inatolewa na ZIPA. Sasa mpaka ZIPA watuhakikishie kwamba mradi fulani umefutwa leseni yake, ndipo upande wa ardhi uchukuwe hatua ya kufuta ile ardhi. Lakini kwa hapa sasa *automatically* ile ardhi itarudi serikalini punde baada ya kufutwa kwa ile leseni ya uwekezaji.

Sasa hili ni jambo jema kwa sababu hakutakuwa tena na ardhi ambayo imebakia bila ya mradi uliokuwa umeendelezwa kwa mujibu wa masharti ambayo imeombewa. Lakini pia itatusaidia kwa mujibu wa masharti ambayo imeombewa, lakini pia itatusaidia kwa ajili ya kuharakisha kumpa mwekezaji mwengine aliyekuwa tayari kuendeleza mradi unaofanana na ule ama vyenginevyo na kuharakisha yale mapato yetu kupatikana vizuri.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kwa mswada wa marekebisho haya utatupunguzia migogoro kule Mahakamani, kwa sababu kuna watu wengine wanaweza wakajua kwamba hawana haki, lakini kwa vile wana haki ya kwenda Mahakamani wakenda tu. Lakini tukiangalia vizuri hasa ile ya Kiingereza katika kifungu cha 3 kinatupa nafasi vizuri ya kwamba jambo ambalo limeamuliwa na Mhe. Rais ambaye ni mtu wa mwisho kwa mujibu wa sheria hii basi haitofikishwa Mahakamani. Lakini pia inamu-*alert* Mhe. Waziri ambaye atakuwa dhamana ya wizara ya ardhi kuwa makini saa zote, kwa sababu uamuzi wake kuna mwengine ambaye

anaangalia kwa maslahi ya umma. Sasa ukiyaangalia yote haya Mhe. Mwenyekiti, utagundua kwamba mswada huu ni mzuri kwa sababu unatibu vizuri zile changamoto ambazo tunazo sasa. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu ili ajibu hoja za wajumbe. Lakini kabla ya kuja yeye nilikuwa naomba niwaambie wajumbe wote waliokuwepo nje waingie ndani kabla hatujakaa kwenye kamati ili tuweze kuupitisha huu mswada na *quorum* itimie. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuingie ndani. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyachangia ndani ya mswada huu.

Lakini pili, niishukuru kwa dhati kabisa michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa kweli, ni michango ambayo wameitoa kwanza wamefahamu ile dhamira ya serikali ya kuleta marekebisho ya mswada, marekebisho ya sheria mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, wametambua na kufahamu matatizo ambayo yalikuwepo ndani ya sheria za sasa, na ndio maana tukaamua kuja na marekebisho ya sheria mbalimbali. Kwa hivyo, nawashukuru na nawapongeza kwa dhati kwa ufahamu wao mkubwa ambao wameuona ndani ya marekebisho ya vifungu hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla mswada wetu huu umechangiwa na wajumbe sita. Mjumbe wa kwanza ni:

Mhe. Machano Othman Said Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, ambaye naye aliwasilisha mapendekezo ya marekebisho kwenye kifungu cha 56. Kwanza, naomba nikubaliane na mapendekezo ambayo yametoka kwenye kamati kama nilivyosema mwanzo nilipokaa na kamati, mengi ambayo wameyatoa yalikuwa ni ya msingi na tulikubaliana ndani ya kamati.

Vilevile, nimshukuru Mhe. Machano Othman Said kwa jadweli lake la marekebisho ya kifungu cha 56, nadhani ametambua na ameona ukakasi uliokuwepo baina ya pale ambapo serikali inatoa ardhi bila ya kupiga tathmini ya ardhi ambayo inaitoa kwa mtu anayempa. Lakini pale serikali inapoamua sasa kuchukua ardhi yake kwa maendeleo ya nchi na kwa maendeleo ya wananchi kwa jumla, basi serikali kulikuwa kuna vifungu ambavyo serikali inaambiwa ilipe thamani ya ardhi ambayo pale ilipotoa haikutathmini thamani yenyewe ya ardhi. Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Machano Othman Said kwa pendekezo lake hilo. Kimsingi nakubaliana nalo, isipokuwa kuna marekebisho madogo naomba niyafanye.

Mhe. Mwenyekiti, pendekezo lake linasema serikali inaweza kupitisha haki ya matumizi ya ardhi kwa msingi wa maslahi ya umma kwa kulipa fidia kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 63 cha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Machano Othman badala ya neno "serikali" tuweke waziri, kwa sababu waziri ndiye aliyepewa mamlaka ya sheria hii ya kutoa ama *lease* au kutoa haki ya matumizi ya ardhi. Sasa Mhe. Machano Othman Said akikubaliana na marekebisho hayo, basi kiujumla nakubaliana na jadweli lake la marekebisho ambayo ameleta. Namshukuru sana kwa kuleta jadweli la marekebisho na hii ndio miongoni mwa kazi ambazo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza nawaomba na nina

wasisitiza waendelee kutusaidia wakati tunajadili na kupitisha miswada hii ya sheria mbalimbali.

Mjumbe wa pili Mhe. Mwenyekiti, alikuwa ni Mhe. Rashid Makame Shamsi, na yeye kwa dhati kabisa namshukuru kwa michango yake yote ambayo aliyoitoa. Kwa ujumla amefafanua mapendekezo yetu yote ambayo ameyaleta, ameona kama kwa sasa ni kweli kwenye baadhi ya mashirika yetu kumekuwa kuna utaratibu sio mzuri wa kulipana maposho na kulipana mishahara, na uwiano baina ya watumishi wa umma na watumishi waliokuwepo kwenye taasisi za serikali haukuwa unalingana.

Sasa mapendekezo ambayo tumeyaleta, kama Mhe. Rashid Makame Shamsi alivyoyaona ni kuweka uwiano sasa kwa baadhi ya mashirika haya yote, kwasababu ndani ya mashirika yenyewe pia hakuna uwiano. Shirika la Umeme lina utaratibu wake, Shirika la Bima lina utaratibu wake. Kwa hivyo, mashirika yote haya ya serikali pia ndani yao wenyewe hakuna uwiano. Sasa marekebisho haya yataweka sawa ule uwiano wa mashirika yote ya serikali, lakini na kile ambacho kinapendekezwa serikali itazingatia haitopishana sana na kile ambacho kinalipwa sasa kwa watumishi wa umma. Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili ni msisitizo alioutoa wa kutukumbusha serikali kuwa na *Government Asset Register*. Nadhani hili alilosema ni jambo kubwa na ni jambo la msingi. Bila ya kuwa na daftari la mali za serikali, basi serikali hatuwezi kujua tuna mali gani na tuna mali ngapi. Kwa hivyo, hili naomba nimuhakikishie kama Wizara ya Fedha na Mipango inalifanyia kazi jambo hili, ili kuhakikisha sasa serikali inajua mali zake zote zilizo kuwepo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ameelezea na kufafanua vizuri kwenye utaratibu huu wa ukodishwaji wa majengo. Ni kweli hivi sasa hali iliyokuwepo imekuwa inatupa wasi wasi na ndio maana tumeamua sasa kuja na marekebisho haya ya sheria, kama sasa Shirika letu la Nyumba halikatazwi kumkodisha mtu jengo lolote la serikali, lakini kwa miaka ikiwa kupindukia zaidi ya miaka 5, basi lazima taarifa zake zije serikalini kwasababu mambo haya pia yanakwenda na mambo ya fedha na yanakwenda na mambo ya ukodishwaji.

Sasa uwekezaji na ukodishwaji wa kawaida wa miaka miwili, mitatu au mitano hilo ruhusa wakodishe kama watakavyoona inafaa. Lakini kwa mikataba ile mikubwa inayokwenda kwa miaka 15, 20 na 25 basi lazima serikali ipewe taarifa kwa sababu serikali ndio mmiliki wa majengo haya. Kwa hiyo, kiujumla namshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa michango yake ambayo ameitoa ya kuboresha mswada huo na yale mapendekezo ambayo ameyatoa kwenye baadhi ya vifungu, vya mswada navyo pia tunakubaliana navyo.

Mheshimiwa Mjumbe wa tatu alikuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali mzee wetu, na yeye pia namshukuru sana kwa pongezi zake kwanza. Lakini pili namshukuru kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kupitia mswada huu mzima na kifungu kimoja kimoja cha marekebisho, namshukuru sana mawazo yake aliyoyatoa tunayaheshimu na yote ambayo ametushauri tunayapokea na tutayafanyia kazi.

Mjumbe wa nne alikuwa ni Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwenyekiti wetu wa Baraza, na yeye pia moja alipendekeza tupunguze miaka, kutoka miaka 33 kuja miaka 30. Pendekezo lake ni zuri, lakini ningemuomba tubakize hii hii miaka 33 kwa sababu nayo pia hii miaka inawasaidia wawekezaji ambao wanaokuja kupata mikopo kule ambapo wanakwenda kuomba

mikopo. Sasa kila miaka ikiwa mingi kidogo na wale ambao wanawakopesha inawapa imani ya kwamba yule mwekezaji ataweza kurudisha zile fedha alizozikopa katika muda muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Mjumbe kwa sasa atuachie tuendelee na kifungu hichi cha miaka 33 ambayo itakuwa sasa inapitiwa kila baada ya muda, hakutokuwa na kutolewa mkataba wa miaka 99 moja kwa moja kama ilivyo sasa. Sasa tutaitoa kwa miaka 33. Lakini tukitaka kuongeza muda basi Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kupitia na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto watafanya tathmini, na kupitia ule uwekezaji ambao umewekwa na wakiridhika nao basi wataongeza muda, lakini kama hawakuridhika basi ule muda wa uwekezaji hautaongezwa, kwa hivyo hiyo ndio dhamira ya kifungu hichi.

Lakini pia ametushauri tuiangalie tena Sheria ya *ZSSF*, na mimi nitawasiliana na wenzangu, ili sasa tujue ni kifungu gani hicho na maeneo gani ambayo yanaleta ugumu katika utekelezaji wake.

Mjumbe wa tano, Mhe. Mwenyekiti alikuwa ni Mhe. Hamza Hassan Juma nimshukuru sana na yeye kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ameyazungumza mengi, na mengi aliyoyazungumza ameyazungumza kutokana na uzoefu wa kazi anayoifanya kupitia kwenye kamati. Kwa hivyo, nimshukuru sana kwa mapendekezo yake mengi ambayo ameyatoa, lakini zaidi ya kutukumbusha kama tupitie tena ile mikataba ya uwekezaji kwenye visiwa vyetu hivi vidogo vidogo. Sisi tunakubaliana nae, kama uwekezaji huu lazima ulete tija kwa serikali lakini pia ulete tija kwa wananchi, hivyo nakubaliana nae.

Vilevile, pia ametushauri tuipitie tena mikataba yote hii ya uwekezaji. Ni kweli hivi sasa kuna wawekezaji *speculators* kwa

lugha ya Kiingereza wanaitwa. Mtu anakuja anawekeza anapeleka mradi wake *ZIPA* anapewa kibali cha kuwekeza lakini baada ya kuwekeza amekuwa sasa dalali wa kuuza ardhi.

Sasa moja ya marekebisho ambayo tunayaleta hivi sasa ni kwamba pale *ZIPA* itapofuta hati ya uwekezaji maana yake ile lease au ule mkataba wa ardhi ambao amepewa nao utafutika moja kwa moja. Sasa kinachofanyika ni kwamba mwekezaji anafutiwa kibali chake *ZIPA*, kwa sababu analipa kodi ya ardhi basi anaendelea kulipa kodi ya ardhi na anabaki na mkataba wetu.

Mapendekezo ambayo tumekuja nayo, ni kwamba kuondoa huo utata ambao upo, mtu aliyepewa uwekezaji awekeze ambaye ameshindwa kuwekeza na akaamua kuweka eneo letu la ardhi na kulipa kodi tu ya ardhi sasa huyo hatutakubaliana nae. Uwekezaji ukifutwa na mkataba wa ardhi aliopewa nao unafutika moja kwa moja, hata kama analipa dola za namna gani kwa serikali. Dhamira ya serikali ni kufungua uwekezaji, kwa sababu kupitia uwekezaji ndio tunapata ajira lakini pia tunaiendeleza na nchi yetu.

Kwa hivyo, mengi ambayo ameyatoa Mhe. Hamza Hassan Juma nakubaliana nayo, lakini pia ametushauri tuangalie kifungu cha 108 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali, bila ya shaka hii pamoja na ile aliyosema Mhe. Shehe Hamad Mattar nayo pia tutaitazama na pale itakapobidi kufanya hivyo tutakuja kufanya marekebisho.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti alikuwa Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na yeye ndio waziri wa sekta naye, nimshukuru kwa pongezi zake na kuyaona yale ambayo mengi yametoka kwao. Lakini nimshukuru kwa pongezi zake, pia nimshukuru kwa kuona haya ambayo yametoka yatawasaidia

zaidi sasa wao kama sekta katika kufanya na kutimiza wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla kama nilivyosema mwanzo nachukua fursa hii kuwashukuru tena sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yote ambayo wameitoa. Nichukue fursa hii kuwaomba wapitishe vifungu vya mswada huu kimoja kimoja bila ya kuwa na buti, bila ya kuwa na *query* yoyote. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa majumuisho yako. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wameujadili mswada huu, naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kupitisha vifungu vya mswada huu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali na mambo mengine yanayohusiana na hayo

Sehemu ya Kwanza

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2	Marekebisho ya Sheria mbalimbali

Sehemu ya Pili

Kifungu cha 3	Kutumika
Kifungu cha 4	Marekebisho ya kifungu Tatu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 5	Marekebisho ya kifungu cha 46
Kifungu cha 6	Marekebisho ya kifungu cha 47 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Kifungu cha 7	Kusomwa
Kifungu cha 8	Marekebisho ya Kifungu cha Sita
Kifungu cha 9	Marekebisho ya kifungu cha nane
Kifungu cha 10	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa kidogo tu nataka ufafanuzi kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu nilimpelekea kwa maandishi na nilichelewa kidogo naomba radhi, lakini kwa faida ya Baraza hili na sheria tunazozitunga kwamba kifungu hichi cha 27 naomba nikinukuu kinasema:

"Waziri anayehusika mara baada ya kupokea taarifa ya mwaka ya kuanzisha ataiwasilisha taarifa kwa Baraza la Mapinduzi kabla hajawasilisha Baraza la Wawakilishi mambo haya yafuatayo".

Mhe. Mwenyekiti, samahani. Mhe. Mwenyekiti, lilikuwa ni suala la maamuzi ya bodi ambayo yatakwenda kwenye Baraza la Mapinduzi, kwa sababu kule kuna sheria ile ya Utumishi wa Umma kifungu cha 9. Sijui kama hii sheria tunayopitisha marekebisho hatukwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma. Ilikuwa kidogo ndio hayo marekebisho nilikuwa nataka kupata ufafanuzi ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma nadhani anazungumzia kifungu cha 9 ambacho kinafanya marekebisho kwenye kifungu cha 8. Kwanza tushakipita 9 kifungu hiki, lakini nitamtolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kinachowekwa hapa kwanza sheria haikatazi bodi ya shirika lolote kufanya maamuzi, lakini mswada huu unaweka maeneo ambapo bodi itakapofanya maamuzi yake kabla yale maamuzi hayakutekelezwa, basi lazima kwanza yafike serikalini na maamuzi yenyewe kwanza ni kuhusu kuwekeza, unapotaka kuwekeza pahala popote, basi lazima kwanza uwekezaji huo upeleke serikalini, ili serikali ijuwe na iweze kuridhia, kwa sababu mashirika yote haya ni mashirika ya umma. Utakaposhindwa kulipa au ule uwekezaji kama hautokwenda vizuri maana yake itakuwa ni dhima ya serikali, kwahivyo, serikali ni lazima ijuwe.

Lakini la pili na unapotaka kukopa, pia lazima serikali nayo ijiridhishe kama shirika linapotaka kukopa lina uwezo pia wa kurudisha lile deni kabla ya uamuzi wa kukopa haukuchukuliwa.

Jengine ni pale inapotaka kupandishwa mishahara na maposho. Nadhani Waheshimiwa Wajumbe wengi hili wameliona na wamelipongeza jambo ambalo limefanywa na serikali. Kama sasa hivi yanayofanyika ni watu wanakaa kwenye vikao wanaamua na wakishakuamua wanaanza utekelezaji wake. Sasa serikali inachofanya sasa hivi ni kwamba nyinyi amueni hamkatazwi kuamua, lakini utekelezaji wake basi lazima nao pia upate ridhaa ya serikali, ndio madhumuni ya kifungu hiki. Mhe. Mwenyekiti, na nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma atakuwa amefahamu na nimuombe tuendelee, nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wako. Tuliona hapa na makatibu kuwa hicho kifungu

kimeshapitishwa, lakini tulitoa hii nafasi ili apate aridhike Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa vile ulisema ni Mwenyekiti wa hiyo Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Nakushukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu. Tuendelee.

Kifungu cha 10 Marekebisho ya Kifungu cha 27 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011

Kifungu cha 11 Kusomwa
Kifungu cha 12 Marekebisho ya Kifungu cha 15
Kifungu cha 13 Marekebisho ya Kifungu cha 29
Kifungu cha 14 Marekebisho ya Kifungu cha 55

Sehemu ya Tano

Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 1 ya 2017

Kifungu cha 15 Kusomwa
Kifungu cha 16 Marekebisho ya Kifungu cha 32

Sehemu ya Sita

Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar Nam. 6 ya 2014

Kifungu cha 17 Kusomwa
Kifungu cha 18 Marekebisho ya Kifungu cha 7

Kifungu cha 19 Marekebisho ya Kifungu cha 26 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Saba

Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi, Nam. 4 ya 2015

Kifungu cha 20 Kusomwa

Kifungu cha 21 Marekebisho ya Kifungu cha 41 pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nane

Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003

Kifungu cha 22 Kusomwa

Kifungu cha 23 Kuongezwa Kifungu kipya cha 9(A) pamoja na marekebisho yake

Jadweli
Mwendo wa Bodi
(Chini ya Kifungu cha 9A)

Kifungu cha 1 Muda wa Mjumbe wa Bodi

Kifungu cha 2 Vikao vya Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 3 Akidi ya Kikao
Kifungu cha 4 Uamuzi wa Bodi
Kifungu cha 5 Kumualika mtu kwenye kikao

Kifungu cha 6	Kumbukumbu za vikao vya bodi
Kifungu cha 7	Utaratibu wa vikao
Kifungu cha 8	Kutaja mgongano wa maslahi
Kifungu cha 9	Katibu wa Bodi
Kifungu cha 10	Kazi za Katibu pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 11	Kamati za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 12	Kujiuzulu na kusita kwa nafasi ya mjumbe
Kifungu cha 13	Nafasi ya Mjumbe kuwa wazi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 14	Posho za Wajumbe pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tisa

Marekebisho ya Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya 2013

Kifungu cha 24	Kusomwa
Kifungu cha 25	Marekebisho ya kifungu cha 2
Kifungu cha 26	Marekebisho ya kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 27	Marekebisho ya kifungu cha 19
Kifungu cha 28	Marekebisho ya kifungu cha 129
Kifungu cha 29	Marekebisho ya kifungu cha 155
Kifungu cha 30	Marekebisho ya kifungu cha 191
Kifungu cha 31	Marekebisho ya kifungu cha 195
Kifungu cha 32	Marekebisho ya kifungu cha 216
Kifungu cha 33	Marekebisho ya kifungu cha 235
Kifungu cha 34	Marekebisho ya kifungu cha 241 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 35	Marekebisho ya kifungu cha 248

Kifungu cha 36 Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 279

Sehemu ya Kumi

Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi na Uondowaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya 2016

Kifungu cha 37 Kusomwa
Kifungu cha 38 Marekebisho ya kifungu cha 27
Kifungu cha 39 Kuongeza kifungu kipya cha 65A

Sehemu ya Kumi na Moja

Marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Viongozi Maalum Nam. 5 ya 2003 Pamoja na Marekebisho yake

Kifungu cha 40 Kusomwa
Kifungu cha 41 Marekebisho ya kifungu cha 6

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Naliomba sasa Baraza lako tukufu liukubali. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba sasa ukubaliwe.

(Mswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba na mimi nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana wachangiaji wote. Lakini pia niwapongeze kamati na nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa hoja yake na majibu yake. Kwahivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe mswada tayari tumeshaupitisha na serikali tuombe kwa Mhe. Rais afanye kwa haraka atie saini mswada huu kwa manufaa ya wananchi na maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha kikao naomba niwatangazie kuwa tukimaliza hapa tunatakiwa twende kwenye ile semina ya *National Insurance Cooperation* hapo juu na baadaye saa 10:00 jioni tutaendelea na ile semina ambayo tulizungumza jana.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niahirishe kikao mpaka kesho saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 07/12/2017 saa 3:00 za asubuhi)